# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

# MWONGOZO WA ELIMU YA MPIGA KURA WA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI WA MWAKA 2025


***Anwani ya Simu**: "UCHAGUZI"*

***Nambari ya Simu:** +255 26-2962345-8*

***Nambari ya Nukushi:** +255 26-2962348*

***Baruapepe:** uchaguzi@inec.go.tz*

***Tovuti:** www.inec.go.tz*

*Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,*

*Uchaguzi House,*

*Eneo la Uwekezaji Njedengwa,*

*Kitalu D, Kiwanja Na. 4,*

*5 Barabara ya Uchaguzi,*

*S.L.P 358,*

***41107 DODOMA.***

YALIYOMO

**DIBAJI** ........ viii

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**1.0 Utangulizi** ........ 1

**1.1 Malengo ya Sura ya Kwanza** ........ 1

**1.2 Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi** ........ 1

1.2.1 Historia ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ........ 2

1.2.2 Muundo wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ........ 3

1.2.3 Majukumu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ........ 3

**1.3 Dira, Dhima na Maadili ya Msingi** ........ 4

1.3.1 Dira ........ 4

1.3.2 Dhima ........ 4

1.3.3 Maadili ya msingi ........ 5

**1.4 Sheria zinazosimamia Uchaguzi Tanzania** ........ 5

**1.5 Mfumo wa Uchaguzi** ........ 5

**1.6 Mzunguko wa Uchaguzi** ........ 6

1.6.1 Kabla ya uchaguzi ........ 6

1.6.2 Wakati wa uchaguzi ........ 7

1.6.3 Baada ya uchaguzi ........ 7

**SURA YA PILI** ........ 9

**2.0 Utangulizi** ........ 9

**2.1 Malengo ya Sura ya Pili** ........ 9

**2.2 Mamlaka ya Tume katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura** ........ 9

**2.3 Elimu ya Mpiga Kura** ........ 10

**2.4 Elimu ya Uraia** ........ 10

**2.5 Ushirikishwaji wa Wadau** ........ 11

**2.5.1 Wapiga kura** ........ 11

2.5.2 Vyama vya siasa ........ 11
2.5.3 Taasisi na asasi za kiraia ........ 12
(i) Vigezo ........ 12
(ii) Njia ya kutuma maombi ya kutoa elimu ya mpiga kura ........ 12
(iii) Viambatisho muhimu ........ 13
(v) Tamko la kutekeleza mwongozo wa elimu ya mpiga kura ........ 13
(vi) Utambulisho wa watoa elimu ya mpiga kura ........ 14
2.5.4 Vyombo vya habari ........ 14
2.5.5 Viongozi wa dini ........ 15
2.5.6 Makundi mbalimbali ........ 15
2.5.6.1 Watu wenye ulemavu ........ 15
2.5.6.2 Wanawake ........ 16
2.5.6.3 Vijana ........ 16
2.5.6.4 Wasiojua kusoma na kuandika ........ 16
2.5.6.5 Wafugaji na wavuvi ........ 17
2.5.6.6 Jamii za wawindaji na waokota matunda ........ 17
2.6 Njia za Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura ........ 17
2.6.1 Mikusanyiko ya watu ........ 18
2.6.2 Mikutano na wadau ........ 18
2.6.3 Vyombo vya habari ........ 18
2.6.4 Magazeti ........ 18
2.6.5 Redio na televisheni ........ 18
2.6.6 Mitandao ya kijamii ........ 18
2.6.7 Tovuti ........ 19
2.6.8 Machapisho ........ 19
2.6.9 Sanaa ........ 19
2.6.10 Gari la elimu ya mpiga kura ........ 19
2.7 Zana za Elimu ya Mpiga Kura ........ 20
2.8 Elimu ya Mpiga Kura katika Magereza na Vyuo vya Mafunzo ........ 20
UTEUZI, PINGAMIZI NA RUFAA ZA WAGOMBEA KITI CHA RAIS,

**UBUNGE NA UDIWANI .......................................................................................21**

**3.0 Utangulizi ........................................................................................................21**

**3.1 Malengo ya Sura ya Tatu ..................................................................................21**

**3.2 Uteuzi wa Wagombea .......................................................................................21**

3.2.1 Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ........................................ 22

3.2.2 Sifa za mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ................................................ 22

3.2.3 Masharti ya uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais........................ 23

**Rais......................................................................................................................................24**

***Angalizo*....................................................................................................................25**

3.2.6 Pingamizi dhidi ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ............ 25

3.2.7 Muda wa kuweka pingamizi ......................................................................................... 25

3.2.8 Sababu za pingamizi .................................................................................................... 26

***Angalizo*....................................................................................................................27**

3.2.9 Uamuzi wa pingamizi ................................................................................................... 27

3.2.10 Mgombea pekee wa kiti cha Rais................................................................................ 28

3.2.11 Kujitoa ugombea......................................................................................................... 28

3.2.12 Kutokuwepo kwa mgombea......................................................................................... 28

3.2.13 Kufariki kwa mgombea ............................................................................................... 29

3.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge ......................................................................................... 29

***Angalizo*....................................................................................................................31**

**Masharti ya uteuzi wa mgombea ubunge ...............................................................31**

**3.3.3 Taratibu za uteuzi wa mgombea ubunge ..........................................................32**

**3.3.4 Pingamizi dhidi ya uteuzi wa wagombea ubunge ...............................................33**

**3.3.5 Muda wa kuweka pingamizi ..........................................................................34**

**3.3.6 Wanaoruhusiwa kuweka pingamizi ..................................................................34**

**3.3.7 Uamuzi wa pingamizi....................................................................................35**

**3.3.8 Kukata rufaa..............................................................................................35**

**3.3.9 Mgombea pekee wa nafasi ya ubunge..............................................................36**

**3.4 Uteuzi wa Wagombea Udiwani ........................................................................37**

3.4.1 Sifa za mgombea udiwani........................................................................................38
3.4.2 Kukosa sifa za kugombea udiwani................................................................................38
3.4.3 Masharti ya uteuzi wa mgombea udiwani ....................................................................40
3.4.4 Taratibu za uteuzi wa mgombea udiwani.....................................................................40
3.4.5 Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea udiwani ..........................................................41
3.4.6 Muda wa kuweka pingamizi .........................................................................................42
3.4.7 Wanaoruhusiwa kuweka pingamizi...............................................................................43
3.4.8 Uamuzi wa pingamizi ...................................................................................................43
3.4.9 Kukata rufaa ................................................................................................................44
3.4.10 Mgombea pekee wa nafasi ya udiwani......................................................................44

**3.5 Kujitoa, Kifo au Kutokuwepo kwa Mgombea.......................................................... 45**
3.5.1 Kujitoa kwa mgombea ..................................................................................................45
3.5.2 Kutokuwepo kwa mgombea...........................................................................................46
3.5.3 Kufariki kwa mgombea ..................................................................................................46

**KAMPENI ZA UCHAGUZI NA KANUNI ZA MAADILI YA UCHAGUZI 48**

**4.0 Utangulizi ............................................................................................................. 48**

**4.1 Malengo ya Sura ya Nne ........................................................................................ 48**

**4.2 Kampeni za Uchaguzi ............................................................................................ 48**

**4.3 Mratibu wa Ratiba za Kampeni za Wagombea Kiti cha Rais na Makamu wa Rais 49**

**4.4 Mratibu wa Ratiba za Kampeni za Wagombea Ubunge ......................................... 50**

**4.5 Mratibu wa Ratiba za Kampeni za Wagombea Udiwani ........................................ 50**

**4.6 Kampeni za Uchaguzi katika Magereza na Vyuo vya Mafunzo .............................. 51**

**4.7 Kanuni za Maadili ya Uchaguzi.............................................................................. 52**

**4.8 Kamati za Maadili ya Uchaguzi.............................................................................. 53**
4.8.1 Kamati ya kata ..............................................................................................................53
4.8.2 Kamati ya jimbo.............................................................................................................53
4.8.3 Kamati ya kitaifa............................................................................................................54
4.8.4 Kamati ya rufaa .............................................................................................................55
4.8.5 Kamati za maadili kwa mgombea pekee wa kiti cha Rais, ubunge au udiwani .....55
4.8.6 Kamati za maadili wakati wa uchaguzi mdogo .................................................... 55

**4.9 Ukiukwaji wa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi** .......... **56**
4.10.1 Muda wa kuwasilisha malalamiko ya ukiukwaji wa kanuni za maadili .......... 57

**SURA YA TANO KUPIGA KURA, KUHESABU KURA, KUJUMLISHA KURA NA KUTANGAZA MATOKEO** .......... **58**

**5.0 Utangulizi** .......... **58**

**5.1 Malengo ya Sura ya Tano** .......... **58**

**5.2 Sifa za Kupiga Kura** .......... **58**

**5.3 Tangazo la Uchaguzi** .......... **59**

**5.4 Vituo vya Kupigia Kura** .......... **60**
5.4.1 Vituo vya kupigia kura katika magereza na vyuo vya mafunzo .......... 60
5.4.2 Muda wa kufungua na kufunga vituo .......... 61

**5.5 Kupiga Kura ya Rais katika Kituo cha Kupigia Kura Tofauti na Kituo Alichojiandikisha Mpiga Kura** .......... **61**
5.5.1 Utaratibu wa maombi ya kupiga kura ya Rais katika kituo cha kupiga kura tofauti na alichojiandikisha mpiga kura .......... 61
5.5.2 Sababu za maombi ya kupiga kura ya Rais katika kituo cha kupigia kura tofauti na alichojiandikisha mpiga kura .......... 62
5.5.3 Utaratibu wa uwasilishaji wa maombi ya kupiga kura ya Rais katika kituo cha kupiga kura tofauti na alichojiandikisha mpiga kura .......... 62

**5.6 Uratibu, Usimamizi na Uendeshaji wa Uchaguzi katika Magereza na Vyuo vya Mafunzo** .......... **64**
5.6.1 Watendaji wa uchaguzi .......... 64
5.6.2 Majukumu ya watendaji wa uchaguzi katika vituo vya kupigia kura ndani ya magereza na vyuo vya mafunzo .......... 65
5.6.3 Watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura kilichopo ndani ya gereza na chuo cha mafunzo .......... 65

**wanaoruhusiwa kupiga kura na aina ya kura watakayopiga** .......... **66**

**5.6.5 Utaratibu wa kuingia katika vituo vya kupigia kura vilivyopo katika magereza na vyuo vya mafunzo** .......... **66**

**5.6.6 Mashauriano kati ya Tume, jeshi la magereza na chuo cha mafunzo** .......... **67**

**5.7 Fomu na Vifaa vya Kupigia Kura** ........ 67

**Fomu na Vifaa vitakavyotumika siku ya kupiga kura** ........ 67

**5.8 Maandalizi Kabla ya Kupiga Kura Kituoni** ........ 71

5.8.1 Utaratibu wa kupiga kura ........ 72

5.8.2 Kuharibika kwa kura ........ 72

**5.9 Kuhesabu Kura** ........ 73

5.9.2 Utaratibu wa kufuata wakati wa kuhesabu kura ........ 74

5.9.3 Kura zitakazohesabiwa kuwa zimekataliwa ........ 75

5.9.4 Uamuzi wa kura kuwa halali au kutokuwa halali ........ 75

5.9.5 Kura zenye mgogoro, kura zilizokataliwa na kura halali ........ 76

**5.10 Taarifa ya Majumuisho ya Kura** ........ 76

5.10.1 Watu wanaoruhusiwa kuingia katika chumba cha kujumlisha kura ........ 77

5.10.2 Utaratibu wa kufuata kabla ya kuanza kujumlisha kura ........ 77

5.10.3 Utaratibu wa kufuata wakati wa kujumlisha kura ........ 78

5.10.4 Kufungana kwa kura ........ 78

5.10.5 Ombi la kurudia kuhesabu kura ........ 79

5.10.6 Matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais ........ 79

5.10.7 Matokeo ya uchaguzi wa Rais ........ 79

**5.11 Wakala wa Upigaji Kura** ........ 81

5.11.1 Majukumu ya wakala wa upigaji kura ........ 81

5.11.2 Sifa za wakala wa upigaji kura ........ 82

5.11.3 Wakala wa upigaji kura au mgombea kuridhika au kutoridhika katika kituo cha kupigia kura ........ 82

5.11.4 Utambulisho wa mawakala wa upigaji kura ........ 83

**WABUNGE NA MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUMU** ........ 84

**6.0 Utangulizi** ........ 84

**6.1 Malengo ya Sura ya Sita** ........ 84

**6.2 Viti Maalumu** ........ 84

**Maalumu** ........ 85

**6.4 Wabunge Wanawake wa Viti Maalumu** ........ 86

6.4.1 Namna ya kupata asilimia 40 ya wabunge wanawake wa viti maalumu ...............86
6.4.2 Kupata asilimia tano (5%) ya kura zote za ubunge ................................................87
6.4.3 Kupata viti maalumu vya ubunge kwa kila chama ..........................................................87

**6.5 Madiwani Wanawake Viti Maalumu ........................................................................ 88**
6.5.1 Uteuzi wa madiwani wanawake wa viti maalumu..........................................................88
6.5.2 Upatikanaji wa madiwani wa viti maalumu ....................................................................88
6.5.3 Upatikanaji wa idadi ya madiwani wa viti maalumu kwa kila chama ..............................88

**SURA YA SABA MAKOSA NA ADHABU WAKATI WA UCHAGUZI ...... 90**

**7.0 Utangulizi ........................................................................................................ 90**

**7.1 Malengo ya Sura ya Saba....................................................................................... 90**

**7.2 Makosa na Adhabu ........................................................................................... 90**

**7.3 Makosa Yanayohusu Uteuzi na Uchaguzi .................................................................. 91**

## DIBAJI

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikitoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo wakati wa Uchaguzi. Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wakati wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025, umeandaliwa na Tume ili kuwezesha taasisi na asasi hizo kutoa elimu iliyokusudiwa.

Mwongozo umefafanua namna ya utoaji wa elimu na mambo muhimu kuhusu mchakato wa uchaguzi ikiwa ni pamoja na uteuzi wa wagombea, kampeni na maadili ya uchaguzi, sifa za kupiga kura, muda wa kufungua na kufunga vituo vya kupiga kura, utaratibu wa kupiga kura, kuhesabu kura, kujumlisha na kutangaza matokeo pamoja na utaratibu wa kuwapata wabunge na madiwani wanawake viti maalumu.

Lengo la mwongozo ni kuwawezesha waelimishaji kutoa elimu inayokidhi matakwa ya Katiba, sheria, kanuni, miongozo na maelekezo yanayotolewa na Tume. Hivyo, Tume inawaasa wadau wenye nia ya kushiriki katika jukumu hili muhimu la kutoa elimu ya mpiga kura kuzingatia mwongozo huu wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yao.

Ni matarajio ya Tume kuwa Mwongozo huu utawawezesha waelimishaji kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na uadilifu.

Jaji (Rufaa) Jacobs C. M. Mwambegele

**MWENYEKITI TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# SURA YA KWANZA

# TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

## 1.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea historia ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi tangu ilipoanzishwa Mwaka 1993 kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Pia, inaainisha dira, dhima, maadili ya msingi, majukumu ya Tume, Sheria zinazosimamia chaguzi za Tanzania, mfumo wa uchaguzi unaotumika nchini pamoja na mzunguko wa uchaguzi.

## 1.1 Malengo ya Sura ya Kwanza

Kumwezesha mwananchi kuelewa kuhusu:- (i) Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

(ii) Historia ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

(iii) Majukumu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

(iv) Mfumo wa Uchaguzi Tanzania.

(v) Sheria zinazosimamia Uchaguzi Tanzania.

(vi) Mzunguko wa Uchaguzi.

**Mambo Muhimu katika Sura Hii**

- **Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;**
- **Dira, Dhima na Maadili ya Msingi;**
- **Majukumu ya Tume; na**
- **Sheria Zinazosimamia Uchaguzi Tanzania.**

## 1.2 Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 74(7) na (11) ya Katiba na kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, Tume ni

idara huru inayojitegemea na inafanya maamuzi yake rasmi kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kwa vikao. Katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba, Tume haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali au maoni ya chama chochote cha siasa.

### 1.2.1 Historia ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Mwaka 1991, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Ali Hassan Mwinyi aliteua Tume chini ya Mwenyekiti Hayati Jaji Mkuu Mstaafu Francis Nyalali. Madhumuni ya Tume hiyo ilikuwa ni kukusanya maoni ya wananchi juu ya kuendelea na mfumo wa chama kimoja au kuwa na mfumo wa vyama vingi vya siasa. Kutokana na ripoti ya Tume hiyo, Ibara ya 3(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ilirekebishwa na kufanya Tanzania kuwa taifa linalofuata mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258 ilitungwa ili kuwezesha usajili wa vyama vya siasa. Pia, Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 zilirekebishwa ili kuondokana na mfumo wa chama kimoja na kuruhusu kufanyika kwa uchaguzi chini ya mfumo wa vyama vingi vya siasa. Baada ya marekebisho hayo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilianzishwa tarehe 13 Januari, 1993.

Mwaka 2021 ulifanyika Mkutano wa Wadau wa Kujadili Hali ya Demokrasia ya Vyama Vingi vya Siasa Nchini Tanzania. Pamoja na mambo mengine, mkutano huo ulitoka na azimio la kuboresha mfumo wa uchaguzi nchini. Hivyo, tarehe 23 Desemba, 2021 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliunda Kikosi Kazi cha kutathmini hali ya demokrasia ili kutoa mapendekezo ya kuboresha masuala ya demokrasia na hali ya kisiasa nchini.

Kikosi Kazi kilitoa mapendekezo ya kufanyika kwa maboresho ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292. Maboresho hayo yalisababisha kutungwa kwa Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na.2 ya Mwaka 2024 na Sheria ya Uchaguzi wa

Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024. Kufuatia kutungwa kwa sheria hizo, jina la Tume ya Taifa ya Uchaguzi lilibadilika na kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

### 1.2.2 Muundo wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Kwa mujibu wa Ibara ya 74(1) na (2) ya Katiba na kifungu cha 5 cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, Tume ina jumla ya Wajumbe saba (7) na Katibu wa Tume ambaye ni Mkurugenzi wa Uchaguzi. Tume inaongozwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti ambao wanatakiwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufani au mtu mwenye sifa ya kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano.

Ibara ya 74(2) ya Katiba, inaweka masharti ya uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume. Katika Uteuzi, Rais wa Jamhuri ya Muungano huzingatia Kanuni ya kuwa endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka sehemu moja ya Muungano, Makamu wake atakuwa ni mtu anayetoka sehemu ya pili ya Muungano.

Kifungu cha 5(2)(b) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, kinaainisha kuwa Rais atateua wajumbe wengine wa Tume kutoka miongoni mwa majina yatakayowasilishwa na Kamati ya Usaili baada ya kufanyiwa usaili. Aidha, katika utekelezaji wa majukumu yake, Tume husaidiwa na Sekretarieti inayoongozwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Tume, kama inavyoelezwa katika Ibara ya 74(7) ya Katiba ikisomwa pamoja na kifungu cha 5(5) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024.

### 1.2.3 Majukumu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi

Majukumu ya Tume yameainishwa katika Ibara ya 74(6) na 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 zikisomwa pamoja na kifungu cha 10 cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024. Majukumu hayo ni: -

(i) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano na Madiwani kwa Tanzania Bara;

(ii) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na Uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara;

(iii) kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge;

(iv) kuteua na kuwatangaza Wabunge Wanawake wa Viti Maalumu katika Jamhuri ya Muungano na Madiwani Wanawake wa Viti maalumu kwa Tanzania Bara;

(v) kuandaa na kusimamia kanuni za maadili ya uchaguzi;

(vi) kutoa elimu ya mpiga kura nchini;

(vii) kuratibu na kusimamia taasisi na asasi zinazotoa elimu ya mpiga kura;

(viii) kualika na kusajili waangalizi wa uchaguzi;

(ix) kuajiri au kuteua watumishi na watendaji wa Tume kwa kadri itakavyohitajika kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 na masharti mengine yatakayowekwa na Tume; na

(x) kutekeleza majukumu mengine yoyote kama yalivyoainishwa kwenye katiba au sheria nyingine yoyote.

### 1.3 Dira, Dhima na Maadili ya Msingi

Katika kutekeleza majukumu yake, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaongozwa na Dira, Dhima na Maadili ya Msingi.

#### 1.3.1 Dira

Uwepo wa mfumo wa uchaguzi unaoaminika na unaohakikisha chaguzi huru na haki.

#### 1.3.2 Dhima

Kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi kwa kuzingatia sheria ili kuimarisha demokrasia kwa manufaa ya wananchi, vyama vya siasa na wagombea.

### 1.3.3 Maadili ya msingi

Tume inazingatia maadili ya msingi yafuatayo: -

(i) uwajibikaji;

(ii) uadilifu;

(iii) ushirikishwaji;

(iv) uwazi; (v) kutopendelea; na (vi) weledi.

## 1.4 Sheria zinazosimamia Uchaguzi Tanzania

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuratibu shughuli za uchaguzi itazingatia: -

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

(ii) Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024 na kanuni zake; na

(iii) Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 na kanuni zake.

Pamoja na sheria tajwa, pia Tume huzingatia sheria zifuatazo: -

(i) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287;

(ii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288;

(iii) Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258;

(iv) Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278;

(v) Sheria ya Uraia, Sura ya 357; na

(vi) Sheria nyingine yoyote ya Tanzania pale itakapohitajika.

## 1.5 Mfumo wa Uchaguzi

Tanzania inatumia mfumo wa uchaguzi ambao mgombea anayepata kura nyingi halali kuliko mgombea mwingine yeyote ndiye hutangazwa kuwa mshindi *(first –past–the post).* Hii, ni kwa mujibu wa Ibara ya 41(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 45(10), 105(1)(a) na 106(1)(a) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024. Aidha, mfumo mwingine unaotumika ni ule wa uwiano wa kura *(proportional representation)* ambao hutumika kupata Wabunge Wanawake wa Viti Maalumu kama

ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 78 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 112 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024.

Pia, mfumo huu hutumika kuwapata Madiwani Wanawake wa Viti Maalumu kwa uwiano wa Viti vya Udiwani vya Kata ambavyo kila Chama kimeshinda katika Halmashauri husika. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 113 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kifungu cha 35(1)(d) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na kifungu cha 24(1)(c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288.

## 1.6 Mzunguko wa Uchaguzi

Kwa mujibu wa Ibara ya 42 (2) na 65 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, zinaelekeza kuwa Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ufanyike kila baada ya kipindi cha miaka mitano (5). Kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani, katika kuendesha shughuli za uchaguzi, Tanzania hutumia utaratibu wa mzunguko wa uchaguzi ambao umegawanyika katika awamu tatu kama ifuatavyo:-

(i) kabla ya uchaguzi;

(ii) wakati wa uchaguzi; na (iii) baada ya uchaguzi.

### 1.6.1 Kabla ya uchaguzi

Shughuli zinazofanyika kabla ya uchaguzi ni pamoja na:-

(i) maboresho na marekebisho ya sheria, kanuni na maelekezo;

(ii) uandaaji wa maadili ya uchaguzi;

(iii) uandaaji wa bajeti;

(iv) ununuzi wa vifaa;

(v) uteuzi wa watendaji;

(vi) utoaji wa mafunzo kwa watendaji;

(vii) uhakiki wa vituo vya kuandikisha wapiga kura;

(viii) uandikishaji wa wapiga kura;

(ix) uandaaji wa kalenda ya uchaguzi na mpango wa utekelezaji;

(x) utoaji wa habari na elimu ya mpiga kura; na

(xi) uhakiki na ugawaji wa majimbo ya uchaguzi.

### 1.6.2 Wakati wa uchaguzi

Katika awamu hii, shughuli zinazofanyika ni: -

(i) uteuzi wa wagombea;

(ii) usuluhishi wa migogoro ya uchaguzi;

(iii) utoaji wa habari na elimu ya mpiga kura;

(iv) uratibu wa kampeni za uchaguzi;

(v) kusimamia na kuratibu utekelezaji wa kanuni za maadili ya uchaguzi;

(vi) usajili wa waangalizi wa uchaguzi;

(vii) uchapishaji wa karatasi za kura;

(viii) mafunzo kwa watendaji wa uchaguzi;

(ix) usambazaji wa vifaa vya uchaguzi;

(x) upigaji kura;

(xi) kuhesabu kura; (xii) kujumlisha kura; na

(xiii) kutangaza matokeo.

### 1.6.3 Baada ya uchaguzi

Katika awamu hii, shughuli zinazofanyika ni: -

(i) tathmini ya uchaguzi mkuu;

(ii) kuandaa taarifa ya uchaguzi mkuu;

(iii) kuandaa na kusimamia chaguzi ndogo;

(iv) ukaguzi wa mapato na matumizi ya fedha na uhakiki wa vifaa vilivyotumika katika uchaguzi mkuu;

(v) kuratibu kesi za uchaguzi;

(vi) marekebisho ya sheria za uchaguzi;

(vii) kupitia na kuboresha mipaka ya majimbo ya uchaguzi;

(viii) kupitia na kuboresha mifumo ya uchaguzi;

(ix) kupitia na kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(x) kupitia na kuboresha muundo wa Tume; na

(xi) kuandaa mpango kazi kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaofuata.

**Maswali ya tafakuri**

1. Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilianzishwa lini?
2. Je, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ina wajumbe wangapi?
3. Taja majukumu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi?
4. Taja shughuli ambazo Tume huzifanya kabla, wakati na baada ya uchaguzi.

# SURA YA PILI

# ELIMU YA MPIGA KURA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza mamlaka ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kutoa elimu ya mpiga kura, wadau wa uchaguzi na umuhimu wao katika kutoa elimu ya mpiga kura, njia na zana zinazotumika kutoa elimu hiyo.

## 2.1 Malengo ya Sura ya Pili

Mwisho wa sura hii mwananchi atakuwa na uelewa kuhusu; (i)

Maana ya elimu ya mpiga kura.

(ii) Tofauti ya elimu ya mpiga kura na elimu ya uraia.

(iii) Mamlaka ya Tume katika kusimamia na kutoa elimu ya mpiga kura.

(iv) Ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi.

(v) Njia na zana zinazotumika kutoa elimu ya mpiga kura.

**Mambo muhimu katika Sura Hii**

- **Elimu ya mpiga kura**
- **Wadau wa uchaguzi**
- **Taasisi na asasi za kiraia**
- **Makundi mbalimbali**
- **Njia na zana za elimu ya mpiga kura**

## 2.2 Mamlaka ya Tume katika kutoa Elimu ya Mpiga Kura

Kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024 na kanuni ya 22 na 23 ya Kanuni za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi za Mwaka 2024, zimeipa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi mamlaka ya kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi zinazotoa elimu hiyo. Jukumu hili limekuwa likitekelezwa na Tume kama ilivyoelekezwa kwa mujibu wa sheria.

## 2.3 Elimu ya Mpiga Kura

Elimu ya mpiga kura ni elimu ambayo hutolewa kwa wananchi kwa lengo la kuwawezesha kuelewa taratibu za mchakato wa uchaguzi, wajibu wao na umuhimu wa kushiriki katika zoezi la uchaguzi. Vilevile, ni elimu isiyokuwa na hisia, ubaguzi wala itikadi za kisiasa, kidini au kikabila katika mchakato wa uchaguzi.

Pia, elimu ya mpiga kura inajibu maswali ya msingi kwa mpiga kura kama vile wapi, lini na muda gani atapigia kura, atarajie nini akifika kituoni, na wapi atapata matokeo ya uchaguzi. Elimu inapowafikia wadau na wapiga kura kwa usahihi na kwa wakati itawafanya wajiamini na hivyo kushiriki kikamilifu katika mchakato wa uchaguzi hatimaye kuwawezesha wananchi kutumia haki yao ya msingi na ya kikatiba katika kujitokeza na kushiriki kuchagua viongozi wao watakaowaongoza ili kujenga demokrasia na utawala bora nchini.

Kipimo kikubwa cha elimu ya mpiga kura ni idadi ya kura zilizoharibika (*invalid ballots),* pamoja na mwitikio wa wapiga kura, kwa maana ya kuangalia kama wapiga kura walipata taarifa za kutosha kuhusu mchakato wa uchaguzi.

## 2.4 Elimu ya Uraia

Elimu ya uraia inahusu haki na wajibu wa raia katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Wakati wa uchaguzi, elimu ya uraia inamsaidia mwananchi kujua wajibu wake, haki yake, nafasi yake na umuhimu wa kushiriki katika mchakato wa uchaguzi ikiwemo kugombea nafasi za uongozi au kushiriki kuchagua kiongozi anayemtaka. Elimu ya uraia ni tofauti na elimu ya mpiga kura ambayo inamwezesha mwananchi kuwafahamu wagombea, kujua sifa za kuwa mpiga kura, wapi, lini na muda wa kupiga kura na taratibu zinazotakiwa kufuatwa awapo katika kituo cha kupigia kura.

Majibu ya maswali haya ndiyo yanayoweza kuongeza ushiriki wa wananchi katika mchakato wa uchaguzi, ambapo kipimo kikubwa cha elimu ya uraia ni mwitikio wa wananchi katika mchakato wa uchaguzi ikiwemo kujitokeza siku ya kupiga kura kwa kuwa elimu hiyo inajibu swali moja tu la **"KWA NINI?"** Elimu ya uraia ni muhimu katika kufanikisha uchaguzi kwa kuwa ina uwezo wa kuongeza idadi ya wapiga kura wanaojitokeza siku ya uchaguzi.

### 2.5 Ushirikishwaji wa Wadau

Wadau wa elimu ya mpiga kura ni watu au taasisi ambazo kwa namna moja au nyingine zina mchango katika kufanikisha uchaguzi. Tume imekuwa ikishirikisha wadau mbalimbali wakati wa uchaguzi katika kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata elimu itakayomuwezesha kuzifahamu taratibu za uchaguzi ili aweze kushiriki vyema zoezi hilo.

Wakati wa uchaguzi, Tume inashirikisha wadau mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na wapiga kura, vyama vya siasa, taasisi na asasi za kiraia, vyombo vya habari, maafisa habari wa halmashauri, waangalizi wa ndani na wa nje wa uchaguzi, taasisi za dini, makundi mbalimbali kama vijana, wanawake, jamii za wafugaji, wavuvi, waokota matunda na wawindaji, watu wenye ulemavu, wasiojua kusoma na kuandika na wazee wa kimila.

#### 2.5.1 Wapiga kura

Kifungu cha 3 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kinatafsiri mpiga kura kuwa ni mtu yeyote mwenye sifa za kupiga kura katika uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya Sheria hiyo. Aidha, kifungu cha 81(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kinaeleza kuwa Wapiga kura ni watu walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Tume imekuwa ikitoa elimu ya mpiga kura nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata kuwafahamu wagombea, kujua sifa za kuwa mpiga kura, kujua wapi, lini na muda wa kupiga kura, kujua taratibu zinazotakiwa kufuatwa wawapo katika kituo cha kupigia kura.

#### 2.5.2 Vyama vya siasa

Tume hufanya mikutano na viongozi wa vyama vya siasa vyenye usajili kamili ili kuwapa taarifa kuhusu zoezi la uchaguzi na kupata maoni yao. Vyama hivyo vina wajibu wa kuwaelimisha na kuwahamasisha wanachama na wafuasi wao, mashabiki na wananchi kujitokeza kushiriki mchakato wa uchaguzi. Aidha, kila chama cha siasa baada ya kupata ridhaa ya wagombea, kina fursa ya kuteua mtu mmoja atakayejulikana kama wakala wa upigaji kura kwa kila kituo ndani ya jimbo au kata ambayo ina mgombea kwa

madhumuni ya kumwakilisha na kulinda maslahi ya mgombea na chama chake katika kituo cha kupigia kura.

### 2.5.3 Taasisi na asasi za kiraia

Tume imekuwa ikiwashirikisha katika hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi kwa kuwa wana uwakilishi katika sehemu kubwa ya jamii. Wakati wa uchaguzi, Tume hufanya mikutano na wadau hawa katika ngazi ya taifa na mikoa ili kuwapa taarifa kuhusu uwepo wa uchaguzi mkuu na kupokea maoni yao. Vilevile, taasisi na asasi za kiraia hupewa mafunzo na kupatiwa Mwongozo unaotumika kutoa elimu ya mpiga kura ili wapate uelewa wa taratibu na miongozo itakayotumika wakati wa zoezi hilo.

Tume hutoa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu hiyo kwa kuzingatia yafuatayo:-

**(i) Vigezo**

(a) iwe imesajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania;

(b) iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;

(c) ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu watatu, wawili wawe Watanzania;

(d) katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;

(e) iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na

(f) iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

**(ii) Njia ya kutuma maombi ya kutoa elimu ya mpiga kura**

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zitatuma maombi Tume kupitia mfumo wa kusajili watazamaji, asasi za kiraia na vyombo vya habari (Accreditation Management System

- AMS) unaopatikana katika anwani ya https://ams.inec.go.tz ndiyo anuani itakayopokea maombi.

**(iii) Viambatisho muhimu**

Taasisi na asasi za kiraia zinapotuma maombi kupitia mfumo wa kusajili watazamaji, asasi za kiraia na vyombo vya habari (Accreditation Management System - AMS) unaopatikana katika anwani ya https://ams.inec.go.tz zinatakiwa kuambatisha vifuatavyo: -

(a) nakala au kivuli cha cheti cha usajili;

(b) nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi ya kiraia;

(c) majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi ya kiraia; na

(d) anwani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake.

**(iv) Taarifa za watendaji wa taasisi au asasi na ratiba ya utekelezaji**

Baada ya kupata kibali cha kutoa elimu hiyo, taasisi na asasi zinatakiwa kuwasilisha Tume:-

(a) taarifa za rasilimali watu watakaotoa elimu ya mpiga kura;

(b) ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa na taasisi au asasi katika halmashauri husika; na

(c) chanzo cha rasilimali fedha watakazotumia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

**(v) Tamko la kutekeleza mwongozo wa elimu ya mpiga kura**

(a) taasisi au asasi ya kiraia iliyopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura itatakiwa kutoa tamko la kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na maelekezo ya Tume wakati wa kutoa elimu hiyo; na

(b) taasisi au asasi ya kiraia iliyopata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi mkuu itapewa nakala ya Mwongozo huu.

(vi) **Utambulisho wa watoa elimu ya mpiga kura**

Baada ya kupata kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura taasisi na asasi za kiraia zitapewa vitambulisho maalumu vya kuwatambulisha watendaji watakaotoa elimu kwa maeneo waliyoomba.

Aidha, katika kuhakikisha kwamba elimu ya mpiga kura inayotolewa na taasisi na asasi za kiraia ndiyo iliyokusudiwa, Tume hufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utoaji wa elimu hiyo.

***Angalizo*:**

**Masharti yanayopaswa kufuatwa na taasisi au asasi wakati wa kutekeleza utoaji wa elimu ya mpiga kura**

Mara baada ya kupata kibali, taasisi au asasi itapaswa kufuata yafuatayo; -

(a) kuzingatia sheria za Tanzania wakati wote wa utoaji wa elimu ya mpiga kura;

(b) kutoa elimu ya mpiga kura katika maeneo iliyoomba;

(c) kufuata Mwongozo huu na maelekezo mengine yanayotolewa na Tume;

(d) kufuata ratiba ya utoaji wa elimu ya mpiga kura kama ilivyowasilisha;

(e) kuhakikisha zana na nyenzo zitakazotumika zinaakisi maudhui yaliyomo katika Mwongozo;

(f) kuhakikisha inatoa elimu ya mpiga kura iliyokusudiwa na Tume;

(g) mtu yeyote haruhusiwi kutoa elimu ya mpiga kura bila idhini ya Tume;

(h) elimu itakayotolewa isiwe na hisia, ubaguzi, itikadi za kisiasa, kidini au kikabila; na

(i) taasisi na asasi za kiraia zitapatiwa mwongozo wa mambo ya kuzingatia wakati wa kutoa elimu ya mpiga kura.

### 2.5.4 Vyombo vya habari

Vyombo vya habari ni miongoni mwa njia za mawasiliano zinazotumika kutoa elimu kwa umma kwa usahihi bila kuwa na mwelekeo wala itikadi za kisiasa, kikanda, kidini au kikabila. Elimu hiyo imekuwa ikitolewa kupitia vipindi vya redio na televisheni, usambazaji wa habari na taarifa kwa umma, taarifa kwa vyombo vya habari na makala za magazeti. Katika kuhakikisha

kuwa elimu hiyo inatolewa kwa usahihi, Tume hufanya mikutano na wanahabari na kuwaelimisha kuhusu taratibu na miongozo ya uchaguzi.

### 2.5.5 Viongozi wa dini

Viongozi wa dini wamekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha waumini na waamini wao kushiriki katika mchakato wa uchaguzi. Viongozi hawa hushirikishwa kwa kupewa elimu kupitia mikutano na wadau kuhusu utaratibu unaopaswa kufuatwa wakati wa uchaguzi, ili waendelee kuwahamasisha wananchi na wapiga kura kushiriki uchaguzi.

### 2.5.6 Makundi mbalimbali

Tume inatambua umuhimu na ushiriki wa makundi mbalimbali katika mchakato wa uchaguzi. Makundi hayo yanahusisha watu wenye ulemavu, wanawake, vijana, wasiojua kusoma na kuandika na makundi ya watu waliojitenga kutokana na shughuli za kiuchumi (wavuvi, wafugaji) mila na desturi (wawindaji na waokota matunda). Hivyo, Tume imekuwa ikiyafikia makundi hayo kupitia wawakilishi, ili wawe sehemu ya elimu kuhusu taratibu za uchaguzi na kuwahamasisha kushiriki katika mchakato huo.

#### 2.5.6.1 Watu wenye ulemavu

Kwa kuzingatia hali zao, watu wenye ulemavu wamekuwa na ushiriki mdogo wakati wa uchaguzi. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na mila potofu katika baadhi ya jamii ambazo haziwapi nafasi ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kundi hili pia linakosa nafasi ya kupata elimu kuhusu uchaguzi, mfano:-

(i) Matumizi ya kifaa cha kupigia kura chenye maandishi ya nukta nundu kwenye vituo (*tactile ballot folder*);

(ii) Matumizi ya kituturi kwamba kinamwezesha mwenye ulemavu wa viungo kupiga kura;

(iii) Kupewa kipaumbele cha kutopanga mstari wafikapo kituoni;

(iv) Kuruhusiwa kwenda na wasaidizi wao; na

(v) Haki, wajibu na umuhimu wa watu wenye ulemavu kushiriki kwenye uchaguzi.

#### 2.5.6.2 Wanawake

Kihistoria ushiriki wa wanawake katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa umekuwa mdogo kutokana na kuwepo kwa mila potofu katika baadhi ya jamii zetu ambazo zinamnyima mwanamke nafasi ya kujitokeza na kushiriki shughuli mbalimbali za kimaendeleo, kiuchumi na kisiasa. Hali hiyo pia imefanya wanawake wasipate elimu kuhusu mchakato wa uchaguzi, mfano;

(i) haki ya kushiriki katika chaguzi kwa kuchagua na kuchaguliwa;

(ii) kipaumbele kwa wajawazito na wenye watoto wachanga; na

(iii) uhuru wa kushiriki mikutano ya kampeni.

#### 2.5.6.3 Vijana

Vijana ni kundi kubwa katika jamii ambalo wapiga kura wapya wanapatikana. Kwa kuwa ushiriki wao katika masuala ya siasa hutegemea jamii inayowazunguka ni rahisi vijana kupata taarifa na elimu sahihi kuhusu mchakato wa uchaguzi lakini pia ni rahisi kuwapotosha panapokuwa na nia ovu. Hivyo, Tume hushirikisha kundi hili kupitia mikutano na wadau, kurasa za mitandao ya kijamii, sanaa na tovuti ili kuwapa taarifa na elimu kuhusu masuala ya uchaguzi.

#### 2.5.6.4 Wasiojua kusoma na kuandika

Kutokana na hali yao ya kutokujua kusoma na kuandika kundi hili limekuwa likikosa elimu kupitia maandiko na machapisho mbalimbali yanayohusu uchaguzi. Hivyo, Tume hutumia njia mbalimbali za utoaji

wa elimu ya mpiga kura ili waweze kupata uelewa kuhusu taratibu na miongozo ambayo itawasaidia kushiriki katika uchaguzi. Njia hizo ni:-

(i) michezo ya kuigiza;

(ii) matamasha;

(iii) vipindi vya redio na runinga;

(iv) machapisho ya picha; na

(v) muziki wenye ujumbe maalumu.

Hivyo, Tume imekuwa ikiyafikia makundi hayo kupitia wawakilishi, ili wawe sehemu ya elimu kuhusu uchaguzi na kuwahamasisha kushiriki katika zoezi hilo.

#### 2.5.6.5 Wafugaji na wavuvi

Kundi la wafugaji na wavuvi ni kundi lililojitenga ambalo huhama kutoka eneo moja kwenda lingine kutokana na shughuli za kiuchumi. Hivyo, hukosa fursa ya kupata elimu ya mpiga kura kupitia njia za kawaida za mawasiliano kama vile mikutano ya wadau, vyombo vya habari n.k. Hivyo, Tume imekuwa ikiyafikia makundi hayo kupitia wawakilishi wao pamoja na kuyafuata katika maeneo wanayofanyia shughuli zao za kiuchumi na kuwaelimisha kuhusu taratibu za uchaguzi.

#### 2.5.6.6 Jamii za wawindaji na waokota matunda

Jamii ya wawindaji na waokota matunda ni jamii zilizojitenga kutokana na mila na desturi zao. Tume imekuwa ikilifikia kundi hili kupitia viongozi wao wa kimila kwa kuzingatia tamaduni za maeneo husika na kulielimisha kuhusu taratibu za uchaguzi.

## 2.6 Njia za Utoaji wa Elimu ya Mpiga Kura

Tume imekuwa ikitekeleza jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura kwa kutumia njia mbalimbali ili wananchi waweze kuelewa taratibu na miongozo inayohusu uchaguzi. Aidha, Tume imekuwa ikizishirikisha taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura ili kutekeleza jukumu hilo. Njia zinazotumika kutoa elimu hiyo ni:-

### 2.6.1 Mikusanyiko ya watu

Tume inatumia maonesho na matamasha mbalimbali kama vile Sabasaba, Nanenane, Mikutano ya Serikali za Mitaa (ALAT), Wiki ya Sheria na Wiki ya Vijana kwa kutoa elimu ya mpiga kura pamoja na kuwapatia wananchi vijitabu na vipeperushi vyenye kuonyesha hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi. Pia, elimu hiyo hutolewa kwenye masoko, gulio, na minada.

### 2.6.2 Mikutano na wadau

Tume hufanya mikutano na wadau mbalimbali ngazi ya Taifa na mikoa ili kuwafahamisha na kuwaelimisha kuhusu mchakato wa uchaguzi. Wadau ambao hushiriki katika mikutano hiyo ni viongozi wa dini, taasisi na asasi za kiraia, viongozi wa vyama vya siasa, wawakilishi wa wanawake, vijana, watu wenye ulemavu, wazee wa kimila , watu wenye ushawishi na vyombo vya habari.

### 2.6.3 Vyombo vya habari

Tume hutumia vyombo vya habari ili kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za uchaguzi. Vyombo hivyo ni: -

### 2.6.4 Magazeti

Tume huandaa makala mbalimbali zenye kuhabarisha na kuelimisha kuhusu taratibu na miongozo ya uchaguzi ambayo huchapishwa katika magazeti. Pia, Tume hutoa taarifa kwa umma kuhusu uchaguzi mkuu kupitia magazeti.

### 2.6.5 Redio na televisheni

Tume hushiriki katika vipindi mbalimbali vya redio na televisheni kuwaelimisha wapiga kura kuhusu taratibu na miongozo ya uchaguzi kwa lengo la kuwahamasisha kushiriki katika zoezi hilo.

### 2.6.6 Mitandao ya kijamii

Tume inatoa elimu ya mpiga kura kupitia kurasa mbali mbali za mitandao ya kijamii ikiwemo Instagram, Threads, X (Twitter), Facebook na YouTube ili iweze kuwaelimisha wapiga kura hususan vijana kuhusu uchaguzi

**Mitandao ya kijamii inayotumiwa na Tume pamoja na anwani zake.**

| Na | Mtandao wa Kijamii | Anuani |
|---|---|---|
| 1. | Instagram | Tumeyauchaguzi_tanzania |
| 2. | Threads | Tumeyauchaguzi_tanzania |
| 3. | X (Twitter) | Tume ya Uchaguzi_TZ |
| 4. | Facebook | Tume huruya TaifayaUchaguzi |
| 5. | YouTube | UCHAGUZI TV |

### 2.6.7 Tovuti

Tume inatoa habari na elimu ya mpiga kura kwa kutumia tovuti yake (www.inec.go.tz) ili kuwaelimisha wananchi na wadau mbalimbali kuhusu uchaguzi.

### 2.6.8 Machapisho

Tume imekuwa ikiandaa vijitabu, mabango, vipeperushi na majarida mbalimbali yenye ujumbe kuhusu mchakato wa uchaguzi. Machapisho hayo hutolewa kwa wananchi ili waweze kupata elimu kuhusu masuala ya uchaguzi.

### 2.6.9 Sanaa

Tume imekuwa ikitumia sanaa mbalimbali ili kuwaelimisha wapiga kura kuhusu mchakato wa uchaguzi. Sanaa hizo ni nyimbo, maigizo, ngonjera, ngoma na vikaragosi ambavyo hutumika katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ili kuwafikia wananchi.

### 2.6.10 Gari la elimu ya mpiga kura

Tume hutumia gari la elimu ya mpiga kura na magari ya matangazo ambayo hupita katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu kama vile vituo vya mabasi, sokoni, minadani na shuleni ili kuwahabarisha na kuwaelimisha wananchi kuhusu uchaguzi.

## 2.7 Zana za Elimu ya Mpiga Kura

Katika kutoa elimu ya mpiga kura kuhusu uchaguzi, Tume hutumia zana zifuatazo:-

(i) machapisho (vijitabu, majarida, vipeperushi na mwongozo wa elimu ya mpiga kura);

(ii) matangazo;

(iii) mabango (*banners, digital billboards, tyre covers na stickers*); na (iv) sanaa (nyimbo, maigizo, *jingles* na ushairi).

## 2.8 Elimu ya Mpiga Kura katika Magereza na Vyuo vya Mafunzo

(i) Tume itapeleka vipeperushi na nyaraka mbalimbali katika magereza na vyuo vya mafunzo kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu kupiga kura.

(ii) Taasisi au asasi iliyoidhinishwa na Tume itaruhusiwa kutoa elimu ya mpiga kura katika magereza na vyuo vya mafunzo kwa njia ya vipeperushi.

(iii) Taasisi au asasi iliyoidhinishwa kutoa elimu ya mpiga kura, itaandaa vipeperushi na kuviwasilisha Tume kwa ajili ya uhakiki na kuviwasilisha Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo.

**Maswali ya tafakuri**

1. Je, ni nani mwenye mamlaka ya kutoa, kusimamia na kuratibu elimu ya mpiga kura nchini Tanzania?
2. Ili asasi ya kiraia iweze kupatiwa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura inatakiwa kuwa na vigezo/sifa gani?
3. Taja wadau wa elimu ya mpiga kura.
4. Taja njia zinazotumika wakati wa kutoa elimu ya mpiga kura.

## SURA YA TATU

## UTEUZI, PINGAMIZI NA RUFAA ZA WAGOMBEA KITI CHA RAIS, UBUNGE NA UDIWANI

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inazungumzia uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais, ubunge na udiwani pamoja na kuelezea sifa za wagombea wa nafasi hizo. Pia, inaelezea hatua zinazotakiwa kufuatwa katika uwekaji wa pingamizi na rufaa kwa wagombea wa nafasi hizo.

### 3.1 Malengo ya Sura ya Tatu

Sura hii inalenga kumwezesha mwananchi kuelewa kuhusu mambo yafuatayo:

(i) Mamlaka inayohusika kufanya uteuzi wa wagombea.

(ii) Sifa za wagombea.

(iii) Masharti ya uteuzi wa wagombea.

(iv) Wanaoruhusiwa kuweka pingamizi dhidi ya wagombea.

(v) Sababu ya pingamizi dhidi ya wagombea.

(vi) Muda wa kuweka pingamizi.

(vii) Rufaa za wagombea.

**Mambo Muhimu katika Sura Hii**

- **Uteuzi;**
- **Wagombea; ☐ Pingamizi; na ☐ Rufaa.**

### 3.2 Uteuzi wa Wagombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 32, 49 na 61 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza siku ya uteuzi ambayo wagombea watawasilisha fomu za uteuzi. Fomu hizo zitawasilishwa kabla ya saa kumi kamili (10:00) alasiri siku

ya uteuzi. Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais utafanywa na Tume. Wagombea wa ubunge na udiwani watateuliwa na msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi.

### 3.2.1 Uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Kwa mujibu wa kifungu cha 32 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kinaeleza kuwa kila unapofanyika uchaguzi wa Rais, kila chama cha siasa kilichosajiliwa na kinachokusudia kushiriki katika uchaguzi wa Rais kitawasilisha kwa Tume jina la mgombea wa kiti cha Rais na jina la mgombea wa nafasi ya Makamu wa Rais wa chama hicho.

Tume kwa kuzingatia kanuni ya 20 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, Tume hufanya uteuzi wa wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais baada ya kujiridhisha kuwa Mgombea amejaza na kutimiza masharti ya ujazaji wa Fomu Na 8A. Aidha, Mgombea atajaza Fomu Na. 10 ya Tamko la Kuheshimu na Kutekeleza Kanuni za Maadili ya Uchaguzi za Mwaka 2025.

### 3.2.2 Sifa za mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Kwa mujibu wa Ibara ya 39(1) na 47(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

(i) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) awe ametimiza umri wa miaka arobaini (40);

(iii) awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;

(iv) awe anazo sifa za kumwezesha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na

(v) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya uchaguzi mkuu awe hajawahi kutiwa hatiani katika Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali.

### 3.2.3 Masharti ya uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Kwa mujibu wa kifungu cha 34(3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, masharti ya uteuzi wa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ni yafuatayo: -

(i) awe amedhaminiwa na wapiga kura wasiopungua mia mbili (200) waliojiandikisha kupiga kura katika kila mkoa kwa mikoa kumi na kati ya hiyo angalau mikoa miwili iwe ya Tanzania Zanzibar. Hii ina maanisha mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais anatakiwa kudhaminiwa na jumla ya wapiga kura wasiopungua elfu mbili (2,000) kutoka mikoa kumi (10).

(ii) awe ameweka dhamana katika ofisi ya Tume ya Shilingi milioni moja (1,000,000/=) za Kitanzania kupitia akaunti ya amana atakayopatiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi siku ya kuchukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipia atawasilisha kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi hati ya malipo (*pay-in slip)* ya benki ili apatiwe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

(iii) awe ametoa tamko kwamba yupo tayari na ana sifa za kuwa mgombea katika uchaguzi.

(iv) awe ameapa mbele ya Jaji kwamba anazo sifa zinazotakiwa na hajapoteza sifa hizo.

### 3.2.4 Wadhamini wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Watakaowadhamini wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais:- (i) wawe wamejiandikisha kuwa wapiga kura katika mikoa hiyo;

(ii) wawe hawajawadhamini wagombea wengine wa kiti cha Rais au Makamu wa Rais;

(iii) si lazima wawe wanachama wa chama kilichompendekeza; wala si lazima wawe wanachama wa chama chochote cha siasa; na

(iv) wawe wamewadhamini wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais kwa kutumia fomu ya uteuzi.

### 3.2.5 Taratibu za uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais

(i) mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais au mpiga kura aliyeidhinishwa na chama cha siasa kwa maandishi atawasilisha kwa Tume barua ya utambulisho kutoka kwa Katibu Mkuu wa chama cha siasa husika na Tume itampa mtu huyo Fomu Na. 8A.

(ii) mgombea wa kiti cha Rais au Makamu wa Rais atawasilisha Tume nakala nne (4) za fomu za uteuzi;

(iii) mgombea atawasilisha picha nne (4) za rangi zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria (*passport size*) zilizopigwa ndani ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (*white background*) na nyuma ya picha hizo liandikwe jina kamili la mgombea, jimbo na chama kilichompendekeza;

(iv) mgombea atawasilisha uthibitisho wa malipo ya dhamana ya kiasi cha Shilingi milioni moja kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 35 cha Sheria;

(v) mgombea atajaza na kusaini Fomu Na. 10 mbele ya Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(vi) Tume ikishapokea fomu za uteuzi na kujiridhisha kuwa mgombea anazo sifa za kugombea itamteua;

(vii) Tume itabandika nakala moja ya fomu ya uteuzi (Fomu Na. 8A) yenye picha ya mgombea, stakabadhi ya malipo na tamko la kuheshimu na kutekeleza kanuni za maadili ya uchaguzi (Fomu Na. 10); na

(viii) kwa wagombea walioteuliwa kabla au ifikapo saa kumi (10:00) alasiri siku ya uteuzi ili ziweze kukaguliwa na iwapo kuna pingamizi liwasilishwe Tume kupitia Fomu Na. 9A. Fomu hiyo ya uteuzi itabandikwa katika sehemu ya wazi inayoonekana nje ya ofisi za Tume.

> ***Angalizo***
>
> Mgombea anaweza kuwasilisha fomu zake Tume kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi kwa ajili ya ukaguzi na pale ambapo pana dosari mgombea ataelekezwa kurekebisha dosari hizo. Mgombea arudishiwe fomu zake mara baada ya kukaguliwa. Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanywa siku iliyotangazwa na Tume, siku ambayo Tume itapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

### 3.2.6 Pingamizi dhidi ya uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais aliyeteuliwa na Tume kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa kifungu cha 37 (3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 22 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 wanaoruhusiwa kuweka pingamizi ni:-

(i) mgombea yeyote wa kiti cha Rais au Makamu wa Rais;

(ii) Msajili wa Vyama vya Siasa; na

(iii) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

### 3.2.7 Muda wa kuweka pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 37(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kikisomwa pamoja na kanuni ya 22 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, muda wa kuweka pingamizi ni kuanzia saa kumi kamili (10:00) alasiri siku ya uteuzi mpaka saa kumi kamili (10:00) alasiri siku inayofuata. Aidha, endapo Msajili wa Vyama vya Siasa anaweka pingamizi, pingamizi hilo litawasilishwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya siku ya uteuzi. Pingamizi litolewe kwa maandishi katika Fomu Na. 9A, libainishe sababu ya pingamizi na kusainiwa na mweka pingamizi.

### 3.2.8 Sababu za pingamizi

Sababu za pingamizi dhidi ya mgombea zinaweza kuwa zozote kati ya hizi zifuatazo:-

(a) si raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;

(b) hajatimiza umri wa miaka arobaini;

(c) hana sifa za kuwa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(d) hana sifa za kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(e) si mwanachama wa chama cha siasa chenye usajili kamili kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258;

(f) hakudhaminiwa na chama cha siasa kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(g) ametiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano (5) kabla ya uchaguzi;

(h) hakudhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika mikoa kumi 10 ya Jamhuri ya Muungano, ikiwemo angalau mikoa miwili (2) ya Tanzania Zanzibar;

(i) hakudhaminiwa na idadi ya wapiga kura inayotakiwa;

(j) hakulipa dhamana ya Shilingi milioni moja (1,000,000/=) za Kitanzania;

(k) hajaambatisha picha kwenye fomu za uteuzi;

(l) hajaapa kwa mujibu wa kifungu cha 34(3)(c) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024;

(m) hakutaja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia katika uchaguzi chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama Vya Siasa tu);

(n) hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024;

(o) hajatoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025; na

(p) ametenda vitendo vilivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama Vya Siasa tu).

***Angalizo***

Pingamizi lolote ni lazima liwekwe kwa maandishi kwa kutumia Fomu Na. 9A, na lazima litiwe saini na mweka pingamizi.

### 3.2.9 Uamuzi wa pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 37(4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 25(6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, Tume, kabla ya kuamua juu ya uhalali wa pingamizi lolote na bila kuchelewa, itamtaarifu mgombea aliyewekewa pingamizi kwa maandishi na itampa mgombea huyo nafasi ya kujibu pingamizi kwa maandishi ndani ya saa ishirini nne (24) tangu kupokea taarifa ya pingamizi. Baada ya kupokea maelezo, Tume itatoa uamuzi wa kukubali au kukataa pingamizi husika na itawataarifu kwa maandishi wahusika kuhusu uamuzi na sababu za uamuzi wa pingamizi hilo. Uamuzi wa Tume kuhusu pingamizi dhidi ya mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais utakuwa ni wa mwisho.

### 3.2.10 Mgombea pekee wa kiti cha Rais

Kwa mujibu wa kifungu cha 38(1),(2) na (3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024, endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa kiti cha Rais aliyeteuliwa;-

(i) Tume itamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee wa kiti cha Rais;

(ii) mgombea huyo atapigiwa kura ya **Ndiyo** au **Hapana** na atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa Rais endapo atapata kura nyingi za Ndiyo zaidi ya kura zote halali zilizopigwa; na

(iii) endapo mgombea huyo atapata kura nyingi za Hapana zaidi ya kura zote halali zilizopigwa, Tume itatangaza siku nyingine ya uteuzi kwa ajili ya uchaguzi wa Rais kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali.

### 3.2.11 Kujitoa ugombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 39 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 32 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, mgombea wa kiti cha Rais anaweza kujitoa kuwa mgombea kwa:-

(i) kuwasilisha yeye mwenyewe barua ya kujitoa kwa Tume na nakala kwa Katibu Mkuu wa chama cha siasa kilichomdhamini kabla ya saa kumi kamili (10:00) alasiri siku ya uteuzi;

(ii) kutoa tamko katika fomu Na. 28 ambayo itasainiwa na mgombea mbele ya Jaji; na

(iii) endapo mgombea atajitoa kugombea baada ya saa kumi kamili (10:00) alasiri ya siku ya uteuzi, chama chake hakitaruhusiwa kuweka mgombea mwingine mbadala na dhamana iliyotolewa na mgombea haitarudishwa.

### 3.2.12 Kutokuwepo kwa mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 40(1)(a) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024, endapo baada ya saa kumi kamili (10:00) alasiri ya siku ya uteuzi hakuna mgombea halali aliyeteuliwa,

Tume mapema iwezekanavyo kupitia notisi katika Gazeti la Serikali, itapanga siku nyingine ya uteuzi.

#### 3.2.13 Kufariki kwa mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 40(1)(b) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024, endapo mgombea yeyote wa kiti cha Rais au Makamu wa Rais atafariki muda wowote baada ya saa kumi kamili (10:00) alasiri ya siku ya uteuzi na kabla ya kumalizika kwa uchaguzi:-

(i) Tume, mapema iwezekanavyo kupitia notisi katika gazeti la serikali, itateua siku nyingine ya uteuzi si zaidi ya siku kumi na nne (14) baada ya tarehe ya kifo ili kutoa muda kwa chama cha siasa kinachohusika kuteua mgombea mwingine kadiri itakavyokuwa; na

(ii) Tume, itapanga siku nyingine ya uchaguzi wa Rais na taratibu husika zitaanza upya, isipokuwa hakutakuwa na uteuzi mpya kwa wagombea wengine wa kiti cha Rais kama wapo.

### 3.3 Uteuzi wa Wagombea Ubunge

Kwa mujibu wa kifungu cha 49 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume itatangaza siku ya uteuzi wa Wabunge kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge katika jimbo. Aidha, endapo uchaguzi huo utasitishwa taratibu za uchaguzi zitaanza upya.

#### 3.3.1 Sifa za mgombea ubunge

Kwa mujibu wa Ibara ya 67 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, mtu yeyote atakuwa na sifa za kuwa mgombea katika uchaguzi wa ubunge au kuchaguliwa kuwa Mbunge kama atakuwa na sifa zifuatazo: -

(i) ni raia wa Jamhuri ya Muungano;

(ii) ametimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(iii) anajua kusoma na kuandika kwa kiswahili au kiingereza;

(iv) ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa; na;

(v) hajawahi kutiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

### 3.3.2 Kukosa sifa za kugombea ubunge

Ibara ya 67 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inaelekeza kuwa mtu hataruhusiwa kugombea ubunge ikiwa:-

(i) ni raia wa nchi nyingine;

(ii) kwa mujibu wa Sheria inayotumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imethibitishwa rasmi kwamba mtu huyo ana ugonjwa wa akili;

(iii) amehukumiwa na mahakama yoyote katika Jamhuri ya Muungano na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa gerezani kwa muda unaozidi miezi sita kwa kukutwa na hatia ya kosa lolote, vyovyote linavyoitwa, linaloambatana na utovu wa uaminifu;

(iv) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi mkuu amehukumiwa na kupewa adhabu ya kifungo kwa kosa linaloambatana na utovu wa uaminifu au kwa kukiuka Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(v) mtu huyo si mwanachama wa chama cha siasa na ambaye hajapendekezwa na chama cha siasa kuwa mgombea;

(vi) mtu huyo ana maslahi yoyote katika mkataba wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wa aina yoyote aliyowekewa miiko maalumu kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge, na iwapo amekiuka miiko hiyo;

(vii) ameshika madaraka ya afisa mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa madaraka ambayo Rais anaweza au anatakiwa kukabidhi kwa Mbunge kwa

mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano au Sheria iliyotungwa na Bunge;

(viii) kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge inayoshughulikia makosa yanayohusika na uchaguzi wa aina yoyote, mtu huyo amezuiliwa kujiandikisha kama mpiga kura au kupiga kura katika uchaguzi wa Wabunge; na

(ix) ni mgombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Angalizo***

Mtu aliyepewa adhabu ya kulipa faini au kifungo na akalipa faini hazuiwi kugombea ubunge. Iwapo atapewa adhabu ya kulipa faini akashindwa na akatumikia kifungo na kukimaliza kabla ya siku ya uteuzi anaruhusiwa kugombea. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 67(7)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Masharti ya uteuzi wa mgombea ubunge**

Kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024, masharti ya uteuzi wa wagombea ubunge ni kama ifuatavyo:-

(i) adhaminiwe kwa maandishi na wapiga kura wasiopungua ishirini na tano (25) walioandikishwa kuwa wapiga kura katika Jimbo linalohusika. Mgombea haruhusiwi kujidhamini yeye mwenyewe. Mpiga kura anatakiwa kudhamini mgombea ubunge mmoja tu;

(ii) Awe ametoa tamko kwamba yupo tayari na ana sifa za kuwa mgombea katika uchaguzi;

(iii) Awe ameapa mbele ya Hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa zinazotakiwa kugombea ubunge na hajapoteza sifa hizo; na

(iv) aweke dhamana ya Shilingi elfu hamsini (50,000/=) za Kitanzania kwa msimamizi wa uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya

halmashauri atakayopatiwa siku akichukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipa atawasilisha hati ya malipo (*pay-in slip)* ya benki kwa msimamizi wa uchaguzi ili apewe stakabadhi ya kukiri mapokezi. Ni muhimu kuhakikisha wagombea wanapewa akaunti namba ya amana ya Halmashauri kwa ajili ya malipo ya dhamana wanapochukua fomu za uteuzi.

### 3.3.3 Taratibu za uteuzi wa mgombea ubunge

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 50 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 23 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, mgombea ubunge aliyependekezwa na chama cha siasa au mpiga kura aliyeidhinishwa na chama cha siasa kwa maandishi, atawasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi barua ya utambulisho kutoka kwa katibu wa chama cha siasa ngazi ya mkoa, wilaya au jimbo na msimamizi wa uchaguzi atampa mtu huyo Fomu Na. 8B.

Mgombea anaweza kuwasilisha fomu zake Tume kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi kwa ajili ya ukaguzi na pale ambapo pana dosari mgombea ataelekezwa kurekebisha dosari hizo. Mgombea arudishiwe fomu zake mara baada ya kukaguliwa. Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanywa siku iliyotangazwa na Tume, siku ambayo Tume itapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

Mgombea awasilishe nakala nne (4) za fomu ya uteuzi kwa msimamizi wa uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) alasiri siku ya uteuzi. Fomu hizo ziwasilishwe pamoja na:-

(i) picha nne(4) za rangi *(passport size)* zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria zenye muonekano mweupe kwa nyuma *(White background)* zilizopigwa ndani ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Nyuma ya picha liandikwe jina kamili la mgombea na chama anachokiwakilisha

(ii) Uthibitisho wa malipo ya dhamana ya Shilingi elfu hamsini (50,000/=) za Kitanzania.

(iii) Fomu Na. 10 ya tamko la kuheshimu na kutekeleza Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025.

Msimamizi wa uchaguzi, kabla au ifikapo saa kumi kamili (10:00) alasiri siku ya uteuzi, atabandika nakala ya fomu ya uteuzi wa mgombea ubunge aliyeteuliwa katika sehemu ya wazi inayoonekana nje ya ofisi yake.

### 3.3.4 Pingamizi dhidi ya uteuzi wa wagombea ubunge

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea ubunge aliyeteuliwa na msimamizi wa uchaguzi kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria. Kwa mujibu wa kifungu cha 53 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024, sababu ya pingamizi inaweza kuwa yoyote kati ya zifuatazo, kwamba mgombea;-

(a) si raia wa Tanzania;

(b) hajatimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(c) hana sifa za kuwa mgombea ubunge;

(d) hawezi kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza;

(e) si mwanachama wa chama cha siasa kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258;

(f) hakudhaminiwa na chama cha siasa kugombea ubunge;

(g) ametiwa hatiani kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi;

(h) hakudhaminiwa na idadi ya wapiga kura inayotakiwa;

(i) hakulipa dhamana ya Shilingi elfu hamsini (50,000/=) za Kitanzania;

(j) hajaambatisha picha katika fomu ya uteuzi;

(k) hajaapa mbele ya hakimu;

(l) hakutaja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia katika uchaguzi chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya siku ya uteuzi);

(m) hajatoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2025;

(n) hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria;

(o) ametenda vitendo alivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 (Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya siku ya uteuzi); na

(p) hakudhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika jimbo husika.

### 3.3.5 Muda wa kuweka pingamizi

Pingamizi dhidi ya mgombea litawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) alasiri siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi. Aidha, endapo Msajili wa Vyama vya Siasa anaweka pingamizi, pingamizi hilo litawasilishwa ndani ya siku kumi na nne baada ya siku ya uteuzi. Pingamizi litawasilishwa kupitia Fomu Na. 9B litaje sababu na litiwe saini na mweka pingamizi.

### 3.3.6 Wanaoruhusiwa kuweka pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 53(3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Pingamizi linaweza kuwekwa na;-

(i) mgombea mwingine wa nafasi hiyo ndani ya jimbo;
(ii) Msajili wa Vyama vya Siasa; au
(iii) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, pingamizi kuhusu gharama za uchaguzi linaweza kuwekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu. Endapo Msajili wa Vyama vya Siasa atawasilisha

pingamizi kwa msimamizi wa uchaguzi, pingamizi hilo litawasilishwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya siku ya uteuzi.

### 3.3.7 Uamuzi wa pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 53(5) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 25 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, msimamizi wa uchaguzi mara baada ya kupokea pingamizi atafanya yafuatayo:-

(i) atamtaarifu kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi; na

(ii) atamtaka kujibu pingamizi kwa maandishi ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu kupokea taarifa ya pingamizi lililowekwa dhidi yake.

Baada ya msimamizi wa uchaguzi kutoa uamuzi wa pingamizi husika atamjulisha kwa maandishi mgombea anayehusika kuhusu uamuzi na sababu ya uamuzi huo.

### 3.3.8 Kukata rufaa

Kifungu cha 53(6) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 zikisomwa pamoja na kanuni ya 29 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, mgombea yeyote wa nafasi ya ubunge ambaye hataridhika na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu uhalali wa pingamizi anaweza kukata rufaa kwa Tume ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu uamuzi huo ulipotolewa kwakuzingatia masharti yafuatayo: -

(i) Rufaa dhidi ya uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu uteuzi wa mgombea ubunge au udiwani zitawasilishwa kupitia Fomu Na. 12 ambazo zitapatikana kwa msimamizi wa uchaguzi. Warufani watajaza nakala tatu za fomu hizo.

(ii) Fomu ziwasilishwe kwa msimamizi wa uchaguzi ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu msimamizi wa uchaguzi alipotoa uamuzi unaopingwa.

(iii) Msimamizi wa uchaguzi atapokea rufaa hizo kwa niaba ya Tume, ambapo baada ya kuzipokea ataandika muda wa kupokea, atazisaini na kugonga muhuri wa msimamizi wa uchaguzi.

(iv) Msimamizi wa uchaguzi ataitaarifu Tume mapema iwezekanavyo kwa njia yoyote ya haraka kuhusu kupokelewa kwa rufaa yoyote.

(v) Pamoja na rufaa hizo, awasilishe fomu ya uteuzi, fomu ya pingamizi na vielelezo vingine vinavyohusiana na rufaa hiyo.

(vi) Tume, kabla ya kufanya uamuzi wa rufaa, inaweza kumuita mtu yeyote kutoa ushahidi, maelezo au ufafanuzi kuhusu rufaa hiyo.

(vii) Uamuzi utakaotolewa na Tume ni wa mwisho na hautahojiwa na mahakama yoyote, isipokuwa kwa njia ya mashauri ya uchaguzi yatakayowasilishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024.

### 3.3.9 Mgombea pekee wa nafasi ya ubunge

Kwa mujibu wa kifungu cha 54(1),(2) na (3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya ubunge aliyeteuliwa, msimamizi wa uchaguzi atamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee wa nafasi ya ubunge.

Baada ya mgombea pekee kutangazwa kuwa mgombea wa nafasi ya ubunge:-

(i) mgombea huyo atapigiwa kura ya **Ndiyo** au **Hapana**. Endapo atapata kura nyingi za Ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa, atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa Mbunge; na

(ii) endapo mgombea pekee atapata kura nyingi za Hapana kati ya kura zote halali zilizopigwa, Msimamizi wa uchaguzi ataitaarifu Tume kuhusu matokeo hayo, kisha Tume itapanga siku nyingine ya uteuzi na upigaji kura kupitia notisi ya Gazeti la Serikali, sio zaidi ya siku arobaini (40) baada ya siku ya uchaguzi.

Aidha, kwa mujibu wa kanuni ya 33 ya Kanuni za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, endapo kabla ya siku ya uchaguzi kutakuwa na mgombea mmoja baada ya wagombea wengine kujitoa, Tume, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee na Tume inaweza kuendelea na utaratibu wa uchaguzi wa mgombea pekee au kutengua siku ya uchaguzi iliyopangwa awali na kupanga siku nyingine ya uchaguzi.

### 3.4 Uteuzi wa Wagombea Udiwani

Kifungu cha 56(1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kinaeleza kuwa kutafanyika uchaguzi wa udiwani katika mamlaka za Serikali za Mitaa kila mwaka wa tano (5) baada ya uchaguzi wa madiwani uliopita, na wakati wowote Halmashauri mpya inapoanzishwa. Aidha, uchaguzi wa madiwani hautafanyika pale ambapo uanzishwaji wa Halmashauri mpya haujabadilisha mipaka ya majimbo ya ubunge.

Kwa kuzingatia kanuni ya 26 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, mgombea udiwani aliyependekezwa na chama cha siasa au mpiga kura aliyeidhinishwa na chama cha siasa kwa maandishi, atawasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi barua ya utambulisho kutoka kwa katibu wa chama cha siasa ngazi ya mkoa, wilaya, jimbo au kata na msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atampa mtu huyo Fomu Na. 8C pamoja na fomu Na.10.

Siku na saa ya uteuzi ni siku itakayotangazwa na Tume kuwa ndiyo siku ambayo wagombea watawasilisha fomu za uteuzi kwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 56 (4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024.

Mgombea udiwani aliyependekezwa na chama cha siasa atawasilisha fomu za uteuzi kwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata kabla ya saa kumi kamili (10:00) alasiri siku ya uteuzi.

### 3.4.1 Sifa za mgombea udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 59 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, sifa za mgombea udiwani ni:-

(i) awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) awe ametimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(iii) awe hajapoteza sifa kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge;

(iv) awe mkazi wa kawaida wa halmashauri anayogombea;

(v) awe anajua kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza;

(vi) awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa chenye usajili kamili; na

(vii) awe na kipato halali kinachomwezesha kuishi.

### 3.4.2 Kukosa sifa za kugombea udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 60 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, mtu hataruhusiwa kugombea udiwani:-

(i) ikiwa ana kiapo cha utii kwa nchi nyingine tofauti na Jamhuri ya Muungano;

(ii) ikiwa katika sheria yoyote inayotumika Tanzania imethibitika kuwa hana akili timamu;

(iii) ikiwa ametiwa hatiani kwa kosa la kukwepa kulipa kodi ndani ya kipindi cha miaka mitano (5) kabla ya uchaguzi;

(iv) endapo amehukumiwa adhabu ya kifo na mahakama yoyote ya Tanzania au amehukumiwa kutumikia kifungo kinachozidi miezi sita gerezani;

(v) endapo yupo kizuizini chini ya amri iliyotolewa chini ya Sheria ya Uwekaji Kizuizini kwa Usalama, Sura ya 361 na amekuwa kizuizini chini ya amri hiyo kwa kipindi kinachozidi miezi sita;

(vi) endapo ameondolewa nchini, kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Uhamisho wa Wahalifu kwa amri iliyotolewa chini ya Sheria hiyo ambayo inaendelea kwa kipindi kinachozidi miezi sita (6);

(vii) iwapo ni sehemu ya, au ni mbia katika shirika, au ni meneja wa kampuni ambayo ni sehemu ya mkataba wowote unaoendelea na mamlaka ya serikali za mitaa ambayo anataka kuchaguliwa na hajatangaza katika magazeti yanayochapishwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza yanayosambazwa ndani ya eneo la mamlaka inayohusika, taarifa inayoelezea aina ya mkataba na maslahi yake au maslahi ya shirika au kampuni katika mkataba;

(viii) ikiwa amepoteza sifa za kuwa mjumbe wa mamlaka ya serikali za

mitaa kwa Sheria hii au chini ya sheria nyingine yoyote;

(ix) ikiwa amepoteza sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya Sheria hii au amepoteza sifa ya kupiga kura katika uchaguzi wowote chini ya Sheria hii au chini ya sheria nyingine yoyote inayohusu makosa ya uchaguzi; na

(x) kwa kuzingatia upekee na ukomo kama Rais anavyoweza kuelekeza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, iwapo anashikilia au anakaimu nafasi katika ofisi yoyote au uteuzi katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano au mamlaka za serikali za mitaa.

***Angalizo:***

Kiongozi wa chama cha siasa haruhusiwi kupendekeza jina lake na kujidhamini mwenyewe.

### 3.4.3 Masharti ya uteuzi wa mgombea udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 62 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, kikisomwa pamoja na kanuni ya 26 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, ili mgombea udiwani aweze kuteuliwa anapaswa atimize masharti yafuatayo:-

(i) awe amedhaminiwa kwa maandishi na wapiga kura wasiopungua kumi (10) walioandikishwa katika kata anayogombea.

(ii) awe ametoa tamko na kuapa mbele ya Hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa za kugombea udiwani na hajapoteza sifa hizo.

(iii) awe ameweka dhamana ya Shilingi elfu tano (5,000/=) za Kitanzania kwa msimamizi wa uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya Halmashauri atakayopatiwa siku ya kuchukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipia atawasilisha hati ya malipo (*pay-in slip)* ya Benki kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apewe stakabadhi ya malipo ya kukiri mapokezi.

### 3.4.4 Taratibu za uteuzi wa mgombea udiwani

Mgombea udiwani aliyependekezwa na chama cha siasa au mpiga kura aliyeidhinishwa na chama cha siasa kwa maandishi, atawasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi barua ya utambulisho kutoka kwa katibu wa chama cha siasa ngazi ya mkoa, wilaya, jimbo au kata na msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atampa mtu huyo Fomu Na. 8C.

Mgombea anaweza kuwasilisha fomu zake Tume kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi kwa ajili ya ukaguzi na pale ambapo pana dosari mgombea ataelekezwa kurekebisha dosari hizo. Mgombea arudishiwe fomu zake mara baada ya kukaguliwa. Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanywa siku iliyotangazwa na Tume, siku ambayo Tume itapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

Mgombea awasilishe nakala nne (4) za fomu ya uteuzi kwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) alasiri siku ya Uteuzi. Fomu hizo ziwasilishwe pamoja na:-

(i) picha nne (4) za rangi *(passport size)* zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria zenye muonekano mweupe kwa nyuma *(white background)* zilizopigwa ndani ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Nyuma ya picha liandikwe jina kamili la mgombea na chama anachokiwakilisha;

(ii) Uthibitisho wa malipo ya dhamana ya Shilingi elfu tano (5,000/=) fedha taslimu za Kitanzania kwa msimamizi wa uchaguzi ngazi ya kata; na

(iii) Fomu ziwasilishwe na mgombea mwenyewe au kiongozi wa chama kilicho mdhamini kwa niaba ya mgombea.

Msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi, kabla au ifikapo saa kumi kamili (10:00) alasiri siku ya uteuzi, atabandika nakala ya fomu ya uteuzi wa mgombea Udiwani aliyeteuliwa katika sehemu ya wazi inayoonekana nje ya ofisi yake.

### 3.4.5 Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea udiwani

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea udiwani aliyeteuliwa na msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa kifungu cha 65 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, sababu ya pingamizi inaweza kuwa yoyote kati ya zifuatazo, kwamba mgombea:-

(i) si raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) hajatimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(iii) hajui kusoma na kuandika kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza;

(iv) si mwanachama wa chama cha siasa chenye usajili wa kudumu;

(v) si mkazi wa kawaida wa halmashauri ambayo kata anayogombea imo;

(vi) ametiwa hatiani na mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi;

(vii) hajadhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika kata husika,

(viii) hajadhaminiwa na wapiga kura wasiopungua kumi (10);

(ix) hakuna uthibitisho kuwa mgombea ameweka dhamana ya Shilingi elfu tano (5,000/=) fedha taslimu za Kitanzania;

(x) hakuwasilisha picha;

(xi) hajaapa mbele ya hakimu;

(xii) hajadhaminiwa na chama cha siasa kilichosajiliwa;

(xiii) hajataja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia katika uchaguzi chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 (Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu);

(xiv) hajatoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ya Mwaka 2025;

(xv) hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria; na

(xvi) ametenda vitendo vilivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama ya Uchaguzi, Sura ya 278 (Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu).

### 3.4.6 Muda wa kuweka pingamizi

Pingamizi dhidi ya mgombea litawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi kabla ya saa kumi kamili (10:00) alasiri siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi. Aidha, endapo Msajili wa Vyama vya Siasa anaweka pingamizi, pingamizi hilo litawasilishwa ndani ya siku kumi

na nne baada ya siku ya uteuzi. Pingamizi litawasilishwa kupitia Fomu Na. 9C litaje sababu na litiwe saini na mweka pingamizi.

### 3.4.7 Wanaoruhusiwa kuweka pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 65(3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, pingamizi linaweza kuwekwa na:-

(i) mgombea mwingine wa nafasi hiyo ndani ya kata;

(ii) msajili wa Vyama vya Siasa; au

(iii) mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aidha, pingamizi kuhusu gharama za uchaguzi linaweza kuwekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya siku ya uteuzi.

### 3.4.8 Uamuzi wa pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 65(4), (5) na (6) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 28(6),(7) na (8) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi, mara baada ya kupokea pingamizi atafanya yafuatayo:-

(i) atamtaarifu kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi;

(ii) atamtaka kujibu pingamizi kwa maandishi ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu kupokea taarifa ya pingamizi lililowekwa dhidi yake;

(iii) endapo msimamizi msaidizi wa uchaguzi ataamua juu ya pingamizi, atawasilisha uamuzi huo kwa msimamizi wa uchaguzi ambaye bila kuchelewa atapitia uamuzi husika na anaweza kukubali au kutengua uamuzi huo; na

(iv) endapo msimamizi wa uchaguzi anakubali pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea, atafuta jina la mgombea huyo katika orodha ya wagombea walioteuliwa na ataitaarifu Tume.

### 3.4.9 Kukata rufaa

Kifungu cha 65(7) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 zikisomwa pamoja na kanuni ya 29 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, mgombea yeyote wa nafasi ya udiwani ambaye hataridhika na uamuzi wa msimamizi wa uchaguzi kuhusu uhalali wa pingamizi anaweza kukata rufaa kwa Tume ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu uamuzi huo ulipotolewa. Kwa utekelezaji bora wa suala hili, Tume imeweka utaratibu ufuatao: -

(i) Rufaa dhidi ya uamuzi ya msimamizi wa uchaguzi kuhusu uteuzi wa mgombea udiwani itawasilishwa kupitia Fomu Na. 12 zitakazopatikana kwa msimamizi wa uchaguzi na zitajazwa nakala tatu.

(ii) Fomu ziwasilishwe kwa msimamizi wa uchaguzi ndani ya saa ishirini na nne (24) tangu kutolewa kwa uamuzi unaopingwa.

(iii) Baada ya kupokea fomu hizo, msimamizi wa uchaguzi ataandika muda wa kupokea, atasaini na kugonga muhuri wa msimamizi wa uchaguzi.

(iv) Ataitaarifu Tume mapema iwezekanavyo kwa njia yoyote ya haraka kuhusu kupokelewa kwa rufaa yoyote.

(v) Pamoja na rufaa hizo, awasilishe fomu ya uteuzi, fomu ya pingamizi na vielelezo vingine vinavyohusiana na rufaa hiyo.

(vi) Tume, kabla ya kufanya uamuzi wa rufaa, inaweza kumuita mtu yeyote kutoa ushahidi, maelezo au ufafanuzi kuhusu rufaa hiyo.

(vii) Uamuzi utakaotolewa na Tume ni wa mwisho na hautahojiwa na mahakama yoyote, isipokuwa kwa njia ya mashauri ya uchaguzi yatakayowasilishwa kwa mujibu wa sheria.

### 3.4.10 Mgombea pekee wa nafasi ya udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 66 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa kiti cha udiwani aliyeteuliwa, msimamizi msaidizi wa uchaguzi

atamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee wa nafasi ya udiwani. Baada ya mgombea pekee kutangazwa kuwa mgombea wa nafasi ya udiwani:-

(i) mgombea huyo atapigiwa kura ya Ndiyo au Hapana. Endapo atapata kura nyingi za Ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa, atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa diwani; na

(ii) endapo mgombea pekee atapata kura nyingi za Hapana kati ya kura zote halali zilizopigwa, msimamizi wa uchaguzi ataitaarifu Tume kuhusu matokeo hayo, kisha Tume itapanga siku nyingine ya uteuzi na upigaji kura kupitia notisi ya Gazeti la Serikali, sio zaidi ya siku arobaini (40) baada ya siku ya uchaguzi.

Aidha, kwa mujibu wa kanuni ya 33 ya Kanuni za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, endapo kabla ya siku ya uchaguzi kutakuwa na mgombea mmoja baada ya wagombea wengine kujitoa, Tume, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atamtangaza mgombea huyo kuwa mgombea pekee na Tume inaweza kuendelea na utaratibu wa uchaguzi wa mgombea pekee au kutengua siku ya uchaguzi iliyopangwa awali na kupanga siku nyingine ya uchaguzi.

## 3.5 Kujitoa, Kifo au Kutokuwepo kwa Mgombea

### 3.5.1 Kujitoa kwa mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 70 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 kikisomwa pamoja na kanuni ya 32 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, mgombea wa nafasi ya ubunge au udiwani anaweza kujitoa kuwa mgombea kwa:-

(i) kutoa taarifa ya maandishi aliyoisaini na kuiwasilisha yeye mwenyewe Tume na nakala kwa tawi la chama cha siasa kilichomdhamini kabla ya saa kumi kamili (10:00) alasiri siku ya uteuzi;

(ii) kutoa tamko katika fomu Na. 28 ambayo itasainiwa na mgombea mbele ya hakimu; na

(iii) endapo mgombea atajitoa kugombea baada ya saa kumi kamili (10:00) alasiri ya siku ya uteuzi, chama chake hakitaruhusiwa

kuweka mgombea mwingine mbadala na dhamana iliyotolewa na mgombea haitarudishwa.

### 3.5.2 Kutokuwepo kwa mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 72 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, endapo baada ya saa kumi kamili (10:00) alasiri ya siku ya uteuzi hakuna mgombea halali aliyeteuliwa, Tume mapema iwezekanavyo kupitia notisi katika Gazeti la Serikali, itasitisha uchaguzi na kupanga siku nyingine isiyozidi siku thelathini (30) baada ya kusitishwa huko, kwa ajili ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi katika jimbo au kata husika na taratibu za uchaguzi katika jimbo au kata hiyo zitaanza upya.

### 3.5.3 Kufariki kwa mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 71 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, endapo mgombea yeyote wa nafasi ya ubunge au udiwani atafariki muda wowote baada ya saa kumi kamili (10:00) alasiri ya siku ya uteuzi na kabla ya kumalizika kwa uchaguzi:-

(i) baada ya kujiridhisha na taarifa hiyo, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atasitisha uchaguzi katika jimbo au kata husika;

(ii) Tume, kwa notisi katika Gazeti la Serikali, itapanga siku nyingine muafaka si zaidi ya siku thelathini (30) baada ya kusitishwa huko kwa ajili ya uteuzi wa wagombea wa uchaguzi katika jimbo au kata na taratibu za uchaguzi katika jimbo au kata hiyo zitaanza upya; na

(iii) isipokuwa kwamba, uteuzi mpya hautafanyika kuhusiana na mgombea mwingine yeyote aliyeteuliwa kihalali katika uteuzi uliopita na kila mgombea atachukuliwa kuwa ameteuliwa kihalali isipokuwa kama atatoa taarifa ya kujitoa.

**Maswali ya tafakuri**

1. Taja sifa za mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais.
2. Taja sifa za mgombea ubunge.
3. Taja sifa za mgombea udiwani.
4. Taja sababu za pingamizi kwa mgombea udiwani.
5. Nani anaruhusiwa kumuwekea pingamizi mgombea wa kiti cha Rais?.
6. Je, ni muda gani mtu anaweza kuweka pingamizi?
7. Je, ikiwa mgombea atajitoa kabla ya uchaguzi nini kitafanyika?
8. Ikiwa mgombea atafariki kabla ya uchaguzi nini kitafanyika?

## SURA YA NNE

## KAMPENI ZA UCHAGUZI NA KANUNI ZA MAADILI YA UCHAGUZI

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza mamlaka ya kisheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kupanga ratiba ya kampeni za uchaguzi, kuratibu kampeni na kusimamia vyama vya siasa kuheshimu Kanuni za Maadili ya Uchaguzi. Aidha, inaeleza taratibu zinazotakiwa kufuatwa iwapo mgombea atajitoa au kufariki wakati wa kampeni.

### 4.1 Malengo ya Sura ya Nne

Sura hii inalenga kumwezesha mwananchi kuelewa mambo yafuatayo;- (i) Maana ya kampeni za uchaguzi.

(ii) Mratibu wa kampeni za uchaguzi.

(iii) Kanuni za maadili ya uchaguzi.

(iv) Kamati za maadili ya uchaguzi.

(v) Mambo yasiyotakiwa kufanywa wakati wa kampeni.

**Mambo Muhimu katika Sura Hii**

- **Kampeni;**
- **Mratibu wa Kampeni;**
- **Kanuni za Maadili ya Uchaguzi; na □ Kamati za Maadili ya Uchaguzi.**

### 4.2 Kampeni za Uchaguzi

Kwa mujibu wa kifungu cha 73 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024, endapo kuna uchaguzi unaoshindaniwa katika jimbo au kata, kampeni za uchaguzi zitaendeshwa na mgombea, chama chake au wakala wake.

Kwa kuzingatia kanuni ya 34 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 ikisomwa pamoja na kipengele cha 2.1 (c) cha Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 muda wa kuanza kampeni utakuwa saa mbili kamili (2:00) asubuhi na

kumalizika saa kumi na mbili kamili (12:00) jioni. Tume hupanga kipindi rasmi cha kampeni kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2024. Kipindi maalumu cha kampeni kinaanzia siku moja (1) baada ya siku ya uteuzi wa wagombea na kuishia siku moja (1) kabla ya siku ya uchaguzi.

### 4.3 Mratibu wa Ratiba za Kampeni za Wagombea Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Kanuni ya 35 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, inaeleza kuwa ratiba ya kampeni za uchaguzi wa kiti cha Rais huratibiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi. Mkurugenzi wa Uchaguzi, kabla ya kuanza kwa kampeni za uchaguzi kuvitaka vyama vya siasa vilivyopendekeza na kudhamini wagombea, kuwasilisha mapendekezo ya ratiba za mikutano ya hadhara ya kampeni ya mgombea siku saba kabla ya siku ya uteuzi.

Ratiba za kampeni zitaonesha tarehe, muda, mkoa, wilaya na mahali ambapo mgombea atafanya kampeni zake. Mkurugenzi wa Uchaguzi baada ya kupokea mapendekezo ya ratiba za kampeni kutoka kwenye vyama vya siasa ataitisha mkutano kwa ajili ya kuratibu ratiba za kampeni. Mkurugenzi wa Uchaguzi ataitisha mkutano wa wagombea wote au mawakala wa vyama vya siasa wanaohusika kwa ajili ya kuandaa ratiba ya mikutano ya kampeni iliyoratibiwa. Baada ya Mkurugenzi wa Uchaguzi kutayarisha ratiba ya kampeni iliyoratibiwa atawapatia nakala hiyo wafuatao:-

(i) vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi wa Rais;

(ii) waratibu wa uchaguzi wa mikoa;

(iii) wakuu wa mikoa ;

(iv) wasimamizi wa uchaguzi;

(v) Inspekta Jenerali wa Polisi kwa madhumuni ya kuhakikisha usalama; na

(vi) wadau wengine wa uchaguzi kadiri itakavyoonekana inafaa.

Chama cha siasa au mgombea anayeshiriki katika uchaguzi atazingatia ratiba ya mikutano ya kampeni inayoratibiwa.Vilevile, utaratibu huu wa kampeni utatumika pia kwa mgombea pekee.

### 4.4 Mratibu wa Ratiba za Kampeni za Wagombea Ubunge

Kwa mujibu wa kanuni ya 35 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, kampeni za uchaguzi wa ubunge huratibiwa na msimamizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo. Kila chama cha siasa au mgombea anapaswa kabla ya kuanza kampeni kuandaa mapendekezo ya ratiba ya kampeni na kuiwasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi. Mapendekezo ya ratiba ya kampeni yataainisha tarehe, muda na mahali mikutano ya kampeni itakapofanyika.

Msimamizi wa uchaguzi baada ya kupokea mapendekezo hayo, ataitisha kikao cha vyama vyote vya siasa vyenye wagombea wa ubunge kwa ajili ya kupitia na kukubaliana kwa pamoja kuhusu mapendekezo ya ratiba.

Nakala za ratiba ya kampeni za wagombea ubunge hupelekwa kwa:-

(a) vyama vinavyoshiriki uchaguzi wa ubunge katika jimbo;
(b) Mkuu wa Wilaya;
(c) Mkuu wa Polisi wa Wilaya husika kwa ajili ya kutoa ulinzi wakati wa mikutano ya kampeni; na
(d) wadau wengine wa uchaguzi kadiri itakavyoonekana inafaa.

Mabadiliko yoyote ya ratiba ya kampeni, yanapaswa kuwasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi ambaye ataitisha mkutano wa vyama vya siasa vyenye wagombea wa ubunge ili kujadiliana na kukubaliana mapendekezo ya mabadiliko yaliyowasilishwa. Chama cha siasa au mgombea anayeshiriki katika uchaguzi atazingatia ratiba ya mikutano ya hadhara ya kampeni inayoratibiwa.Vilevile, utaratibu huu wa kampeni utatumika pia kwa mgombea pekee.

### 4.5 Mratibu wa Ratiba za Kampeni za Wagombea Udiwani

Ratiba ya kampeni ya uchaguzi wa udiwani huratibiwa na msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata. Kila chama cha siasa au mgombea

anapaswa kabla ya kuanza kampeni kuandaa mapendekezo ya ratiba ya kampeni na kuiwasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi. Mapendekezo ya ratiba ya kampeni yataainisha tarehe, muda na mahali mikutano ya kampeni itakapofanyika.

Msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata baada ya kupokea mapendekezo hayo, ataitisha kikao cha vyama vyote vya siasa vyenye wagombea wa udiwani kwa ajili ya kupitia na kukubaliana kwa pamoja kuhusu mapendekezo ya ratiba.

Nakala za ratiba ya kampeni za wagombea udiwani hupelekwa kwa:-

(a) vyama vinavyoshiriki uchaguzi wa udiwani katika kata;
(b) Mkuu wa Wilaya;
(c) Mkuu wa Polisi wa Wilaya husika kwa ajili ya kutoa ulinzi wakati wa mikutano ya kampeni; na
(d) wadau wengine wa uchaguzi kadiri itakavyoonekana inafaa.

Mabadiliko yoyote ya ratiba ya kampeni, yanapaswa kuwasilishwa kwa msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata ambaye ataitisha mkutano wa vyama vya siasa vyenye wagombea wa udiwani ili kujadiliana na kukubaliana mapendekezo ya mabadiliko yaliyowasilishwa. Chama cha siasa au mgombea anayeshiriki katika uchaguzi atazingatia ratiba ya mikutano ya hadhara ya kampeni iliyoratibiwa. Vilevile, utaratibu huu wa kampeni utatumika pia kwa mgombea pekee.

### 4.6 Kampeni za Uchaguzi katika Magereza na Vyuo vya Mafunzo

(i) Mikutano ya kampeni za uchaguzi haitafanyika ndani ya magereza na vyuo vya mafunzo:

Isipokuwa, vyama vya siasa au mgombea, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, anaweza kuandaa vipeperushi na kuviwasilisha Tume kwa ajili ya uhakiki.

(ii) Tume, baada ya kujiridhisha na maudhui ya vipeperushi husika, itaviwasilisha Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya kuvisambaza.

**4.7 Kanuni za Maadili ya Uchaguzi**

Kanuni za maadili ya uchaguzi ni makubaliano ya pamoja baina ya Vyama vya Siasa, Serikali na Tume yanayoeleza mambo yanayotakiwa au yasiyotakiwa kufanywa wakati wa kampeni za uchaguzi, kupiga kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Pamoja na mambo mengine, Kanuni hizi zinahusu kuheshimiana, kuzingatia ratiba za kampeni, kuelimisha wanachama wa vyama vya siasa katika misingi ya kuelewa sera za vyama husika, kutojenga chuki, kushirikiana na kutobeba silaha za aina yoyote katika mikutano ya kampeni.

Watendaji wa uchaguzi wanapaswa kusimamia na kuendesha uchaguzi kwa mujibu wa sheria, kanuni, maelekezo ya Tume na kuzingatia uwazi na uadilifu. Aidha, vyama vya siasa vinaelekezwa kuzingatia Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025.

Msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata baada ya kupata maelekezo kutoka Tume ataunda kamati za maadili katika ngazi ya jimbo au kata. Hivyo, anatakiwa kuvitaarifu vyama vya siasa na Serikali kuwasilisha majina ya wajumbe siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi.

Kamati hizo zitasimamia na kushughulikia malalamiko yanayotokana na ukiukwaji wa maadili wakati wa kampeni za uchaguzi kuanzia hatua ya kuanza kwa kampeni hadi kukamilika kwa kampeni za uchaguzi. Vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi vina wajibu wa kuhakikisha vinatekeleza makubaliano ya kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi ili kuhakikisha kuwa kampeni zinafanyika kwa amani na utulivu.

### 4.8 Kamati za Maadili ya Uchaguzi

Sehemu ya Tano ya Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, inaelezea Kamati za Maadili ya Uchaguzi ambazo zitashughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa maadili wakati wa kampeni. Kamati hizo ni:-

#### 4.8.1 Kamati ya kata

Kamati hii itasikiliza malalamiko yanayohusu ukiukwaji wa maadili kwenye uchaguzi wa udiwani katika kata husika na itaundwa na msimamizi msaidizi wa uchaguzi baada ya kupata maelekezo kutoka Tume. Kamati hii itaundwa na: -

(i) msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata ambaye atakuwa mwenyekiti wa kamati;

(ii) mjumbe mmoja kutoka kila chama cha siasa kinachoshiriki katika uchaguzi kwenye kata husika ambaye atawasilisha barua ya utambulisho kwa mwenyekiti wa kamati kutoka kwa katibu wa wilaya au kata wa chama husika;

(iii) mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi na katibu tawala wa wilaya husika;

(iv) katibu wa kamati atatoka katika ofisi ya msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata; na

(v) wakati wa kikao cha kamati, katibu atachukua muhtasari wa kikao na atawajibika kutunza kumbukumbu za vikao.

#### 4.8.2 Kamati ya jimbo

Kamati hii itakuwa na mamlaka ya kusikiliza malalamiko ya ukiukwaji wa maadili kwenye uchaguzi wa ubunge katika jimbo husika pamoja na kusikiliza rufaa kutoka kamati ya maadili ngazi ya kata. Kamati hii itaundwa na:-

(i) msimamizi wa uchaguzi katika jimbo ambaye atakuwa mwenyekiti wa kamati;

(ii) mjumbe mmoja kutoka kila chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi katika jimbo husika ambaye atawasilisha barua ya utambulisho kwa mwenyekiti wa kamati kutoka kwa katibu wa wilaya au mkoa wa chama husika;

(iii) mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali ambaye atateuliwa kwa maandishi na katibu tawala wa wilaya husika; na

(iv) katibu wa kamati ambaye atakuwa ni msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo.

Wakati wa kikao cha Kamati, katibu atachukua muhtasari wa kikao na atawajibika kutunza kumbukumbu za vikao.

#### 4.8.3 Kamati ya kitaifa

Kamati hii itakuwa na mamlaka ya kusikiliza malalamiko ya ukiukwaji wa maadili kwenye uchaguzi wa Rais na rufaa kutoka kamati ya jimbo. Kamati hii itaundwa na:-

(i) Mjumbe mmoja wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ambaye atakuwa mwenyekiti wa kamati;

(ii) mwakilishi mmoja kutoka kila chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi wa Rais. Aidha, mwakilishi huyo atapaswa kuwasilisha kwa mwenyekiti wa kamati barua ya uteuzi kutoka kwa Katibu Mkuu wa chama husika;

(iii) mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali atakayeteuliwa kwa maandishi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu; na

(iv) Katibu na katibu msaidizi wa kamati kutoka miongoni mwa maafisa waandamizi wa sekretarieti ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Wakati wa kikao cha kamati, katibu au katibu msaidizi atachukua muhtasari wa kikao na atawajibika kutunza kumbukumbu za vikao.

### 4.8.4 Kamati ya rufaa

Kamati hii itakuwa na mamlaka ya kusikiliza rufaa kutoka Kamati ya Kitaifa na itaundwa na:-

(i) Mwenyekiti ambaye ni Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;

(ii) Makamu Mwenyekiti ambaye ni Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;

(iii) mjumbe mmoja kutoka kila chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi wa Rais ambaye ni mwenyekiti au katibu mkuu au mwakilishi wa chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi wa Rais;

(iv) mjumbe mmoja atakayeiwakilisha Serikali ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu au mwakilishi wake; na

(v) Katibu wa kamati ambaye ni Mkurugenzi wa Uchaguzi au mwakilishi wake na katibu msaidizi wa kamati ambaye ni miongoni mwa maafisa waandamizi wa sekretarieti ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Wakati wa kikao cha kamati, katibu au katibu msaidizi atachukua muhtasari wa kikao na atawajibika kutunza kumbukumbu za vikao.

### 4.8.5 Kamati za maadili kwa mgombea pekee wa kiti cha Rais, ubunge au udiwani

Endapo kuna mgombea pekee wa kiti cha Rais, ubunge au udiwani kamati za maadili zilizoanishwa katika aya ya 5.1 ya Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 zitatumika na utaratibu ulioanishwa katika sehemu hii utatumika. Isipokuwa kwamba kamati hizo zitaundwa na mjumbe mmoja kutoka kwenye chama chenye mgombea pekee, Serikali na Tume.

### 4.8.6 Kamati za maadili wakati wa uchaguzi mdogo

Kutakuwa na Kamati za Maadili wakati wa uchaguzi mdogo kama ifuatavyo:

-

(i) endapo uchaguzi mdogo unafanyika katika kata, kamati itabaki kama ilivyo katika aya ya **4.8.1** ya Mwongozo huu na itaundwa

kamati ngazi ya jimbo kwa ajili ya kupokea rufaa kutoka ngazi ya kata, na

(ii) endapo kutakuwa na uchaguzi mdogo wa ubunge, kamati itakayotumika ni kama ilivyo katika aya ya **4.8.2** ya Mwongozo huu na itaundwa kamati ya kitaifa kwa ajili ya kupokea rufaa kutoka ngazi ya jimbo.

### 4.9 Ukiukwaji wa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi

Miongoni mwa matukio ya ukiukwaji wa Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ni pamoja na:

(i) lugha za kashfa na matusi kwa wagombea na viongozi wa vyama vya siasa wakati wa kampeni;

(ii) kuzidisha muda wa kampeni;

(iii) ukiukwaji wa ratiba ya kampeni;

(iv) maandamano ya wafuasi wa vyama vya siasa yasiyokuwa na kibali kabla na baada ya kampeni;

(v) wafuasi wa vyama vya siasa kuharibu mabango ya wagombea wa vyama vingine;

(vi) baadhi ya watendaji wa Serikali kuingilia shughuli za vyama vya siasa;

(vii) vurugu dhidi ya vyama na wagombea katika baadhi ya maeneo;

(viii) kubandika picha za wagombea juu ya picha za wagombea wa vyama vingine;

(ix) wafuasi wa vyama vya siasa na wagombea kuingilia mikutano ya wagombea wa vyama vingine; na

(x) kutoa kauli zisizoweza kuthibitishwa.

### 4.10 Uwasilishwaji wa Malalamiko ya Ukiukwaji wa Kanuni za Maadili

Mgombea yeyote, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Serikali au chama kilichosaini Kanuni za Maadili ya Uchaguzi na kuweka mgombea iwapo kinaamini kwamba Kanuni za Maadili ya Uchaguzi zimekiukwa kitawasilisha malalamiko yake kwa mwenyekiti wa kamati ya maadili ya uchaguzi katika

ngazi husika kwa maandishi. Aidha, malalamiko kuhusu ukiukwaji wa maadili kwa mgombea pekee yatawasilishwa na Tume au Serikali.

Isipokuwa kwamba changamoto au malalamiko yoyote kuhusiana na mchakato au taratibu za uchaguzi yatakayojitokeza siku ya kupiga kura katika kituo cha kupigia kura, yatawasilishwa kwa maandishi kwa msimamizi wa kituo kupitia kwa wakala wa upigaji kura.

### 4.10.1 Muda wa kuwasilisha malalamiko ya ukiukwaji wa kanuni za maadili

Malalamiko yoyote yatakayotokea yatawasilishwa kwa maandishi kwa mwenyekiti wa kamati ya maadili ya uchaguzi ya ngazi husika ndani ya saa sabini na mbili (72) tangu kutokea kwa tukio linalololalamikiwa.

**Maswali ya tafakuri**

1. Maadili ya uchaguzi ni nini?
2. Nani huratibu kampeni za wagombea kiti cha Rais?
3. Nani huandaa maadili ya uchaguzi?
4. Nini kazi za kamati za maadili?
5. Ni mambo gani yanasababisha ukiukwaji wa maadili ya uchaguzi?

## SURA YA TANO

## KUPIGA KURA, KUHESABU KURA, KUJUMLISHA KURA NA KUTANGAZA MATOKEO

### 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa ufafanuzi kuhusu utaratibu unaosimamia zoezi la kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo. Pia, inaainisha sifa za mpiga kura na kutoa ufafanuzi juu ya uteuzi wa watendaji wa uchaguzi na maelezo kuhusu vituo vya kupigia kura na vifaa vinavyotumika wakati wa uchaguzi.

### 5.1 Malengo ya Sura ya Tano

Sura hii inamwezesha mwananchi kuelewa mambo yafuatayo:-

(i) Tangazo la uchaguzi.

(ii) Fomu na vifaa vya kupigia kura na matumizi yake.

(iii) Utaratibu wa kupiga kura, kuhesabu na kutangaza matokeo.

(iv) Mawakala wa vyama vya siasa.

(v) Mambo yasiyotakiwa kufanyika siku ya kupiga kura.

(vi) Sifa za kupiga kura.

**Mambo Muhimu katika Sura Hii**

- **Tangazo la uchaguzi;**
- **Vituo vya kupigia kura;**
- **Kupiga kura;**
- **Kuhesabu kura;**
- **Kujumlisha kura;**
- **Kutangaza matokeo; na**
- **Mawakala wa vyama vya siasa.**

### 5.2 Sifa za Kupiga Kura

Ili mtu aweze kupiga kura anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

(i) awe amejiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(ii) awe ana Kadi ya Mpiga Kura iliyotolewa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi; na

(iii) awe katika kituo alichojiandikisha kupiga kura au amepata kibali cha kupiga kura katika kituo cha kupigia kura tofauti na kituo alichojiandikisha kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 na Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025.

Msimamizi wa kituo, msimamizi msaidizi wa kituo, karani mwongozaji na wakala wa upigaji kura ambaye kutokana na majukumu yake katika uchaguzi hataweza kupiga kura katika kituo alichojiandikisha, atapewa kibali maalumu (Fomu Na. 18) cha kumwezesha kupiga kura katika kituo atakachofanyia kazi. Endapo msimamizi wa kituo, msimamizi msaidizi wa kituo, karani mwongozaji na wakala wa upigaji kura anayehusika atapangiwa kufanya kazi kwenye kata tofauti na aliyojiandikisha hatapiga kura ya diwani.

Vilevile, atakayepangiwa katika jimbo tofauti na alilojiandikisha, hatapiga kura ya mbunge wala diwani bali atapiga kura ya Rais tu. Aidha, mgombea atapatiwa kibali maalumu (Fomu Na. 19) ambacho kitamwezesha kupiga kura katika kituo chochote katika jimbo au kata anayogombea.

**5.3 Tangazo la Uchaguzi**

Kwa mujibu wa kifungu cha 69(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, msimamizi wa uchaguzi atatoa tangazo la uchaguzi katika jimbo na kata siku nane (8) kabla ya siku ya kupiga kura ili wapiga kura waweze kufahamu mahali, tarehe na siku ya kupiga kura. Aidha, tangazo hilo litabandikwa katika kila kituo cha kupigia kura likionesha yafuatayo:-

(a) tarehe ya kupiga kura;

(b) saa ya kufungua na kufunga vituo vya kupigia kura;

(c) sehemu ambazo waliojiandikisha kupiga kura watapiga kura; na (d) mfano wa karatasi za kura ambazo hutolewa na Tume.

Wakati wa kutoa tangazo la uchaguzi ni vyema yakabandikwa mabango ya hadhari na maelekezo kwa wapiga kura katika vituo vya kupigia kura na kwenye maeneo yenye watu wengi, mfano sokoni. Vilevile, msimamizi wa

uchaguzi anatakiwa kubandika mabango mshale kwenye barabara kuu na njia za kuingilia vituoni katika hali itakayowezesha wapiga kura kutambua vituo vya kupigia kura vilipo. Tangazo la uchaguzi lisainiwe na msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya jimbo au kata.

### 5.4 Vituo vya Kupigia Kura

(i) Vituo vilivyotumika kuandikishia wapiga kura ndivyo vitakavyotumika kupigia kura.

(ii) Idadi ya wapiga kura watakaopiga kura katika kituo itapangwa na Tume, ikiwa wapiga kura ni wengi katika vituo vya kuandikisha wapiga kura Tume inaweza kugawa wapiga kura katika vituo A, B, C. Kwa mfano, ikipangwa idadi ya wapiga kura kwa kituo ni 450 na walioandikishwa ni wapiga kura 1300, kituo hicho kitagawanywa mara tatu, kituo A wapiga kura 450, kituo B wapiga kura 450 na kituo C wapiga kura 400.

(iii) Vituo vya kupigia kura havitakiwi kuwekwa kwenye ofisi za chama chochote cha siasa, majengo ya ibada, vituo au kambi za polisi, kambi za jeshi, nyumba za viongozi au mashabiki wa vyama vya siasa.

(iv) Kutakuwa na mabango mshale yatakayobandikwa kwenye barabara kuu na njia za kuelekea vilipo vituo vya kupigia kura.

#### 5.4.1 Vituo vya kupigia kura katika magereza na vyuo vya mafunzo

(i) Tume, baada ya kushauriana na Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo itapanga vituo vya kupigia kura katika magereza na vyuo vya mafunzo.

(ii) Vituo vya kupigia kura vilivyopangwa katika magereza na vyuo vya mafunzo vitakuwa kwenye ngome au uzio kwa mujibu wa Sheria ya Magereza na Sheria ya Chuo cha Mafunzo, isipokuwa kama itaamuliwa vinginevyo kutokana na mazingira ya wakati na eneo husika.

(iii) Vituo vya kupigia kura ndani ya magereza na vyuo vya mafunzo vitakuwa sehemu ya vituo vya kupigia kura katika eneo la uchaguzi la sehemu husika.

(iv) Tume itavipatia vyama vya siasa idadi ya wapiga kura walioandikishwa kwa kila kituo cha kupigia kura katika magereza na vyuo vya mafunzo.

(v) Utaratibu wa kupiga kura, kuhesabu na kubandika matokeo ya kituo cha kupigia kura pamoja na kujumlisha matokeo utazingatia masharti ya Sheria na Kanuni zinazosimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani.

### 5.4.2 Muda wa kufungua na kufunga vituo

(i) Siku ya uchaguzi vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa moja kamili (1:00) asubuhi na kufungwa saa kumi kamili (10:00) alasiri; na

(ii) Kwa upande wa magereza na vyuo vya mafunzo vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa mbili kamili (2:00) asubuhi na kufungwa saa tisa kamili (9:00) alasiri.

## 5.5 Kupiga Kura ya Rais katika Kituo cha Kupigia Kura Tofauti na Kituo Alichojiandikisha Mpiga Kura

Kwa mujibu wa kifungu cha 42 (3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume inaweza kutoa maelekezo na kuweka utaratibu ambao mtu anaweza, katika siku ya uchaguzi wa Rais, kuruhusiwa kupiga kura katika kituo cha kupigia kura tofauti na kile alichojiandikisha.

### 5.5.1 Utaratibu wa maombi ya kupiga kura ya Rais katika kituo cha kupiga kura tofauti na alichojiandikisha mpiga kura

Kwa kuzingatia kanuni ya 48(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, utararibu wa maombi ya mpiga kura kupiga kura ya Rais katika kituo cha kupigia kura tofauti na kituo alichojiandikisha utakuwa;-

(i) Siku arobaini (40) kabla ya siku ya uchaguzi, Tume itatoa tangazo kuwaalika wapiga kura walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi au Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kuwasilisha maombi ya kupiga kura ya Rais katika vituo vya kupigia kura tofauti na vituo walivyojiandikisha.

(ii) Mpiga kura anayekusudia kupiga kura ya Rais katika kituo cha kupigia kura tofauti na kituo alichojiandikisha, atawasilisha maombi ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya Tume kutoa tangazo.

### 5.5.2 Sababu za maombi ya kupiga kura ya Rais katika kituo cha kupigia kura tofauti na alichojiandikisha mpiga kura

(i) biashara au safari ya muda mrefu katika eneo husika;

(ii) kuwa masomoni au likizo ya masomo;

(iii) kuhamishwa kituo cha kazi;

(iv) kuwa katika matibabu na mpiga kura huyo awe anaweza kufika katika kituo cha kupigia kura;

(v) kuhamishwa makazi;

(vi) kuhukumiwa kutumikia adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita gerezani au katika chuo cha mafunzo;

(vii) kuhamishwa gereza au chuo cha mafunzo kwa mfungwa au mwanafunzi wa chuo cha mafunzo anayetumikia adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita;

(viii) kumaliza kutumikia kifungo gerezani au katika chuo cha mafunzo; au

(ix) sababu nyingine yoyote ambayo Tume itaona inafaa.

### 5.5.3 Utaratibu wa uwasilishaji wa maombi ya kupiga kura ya Rais katika kituo cha kupiga kura tofauti na alichojiandikisha mpiga kura

(i) maombi yatawasilishwa kupitia Fomu Na 29;

(ii) fomu za maombi zitatolewa na kurejeshwa kwa msimamizi wa uchaguzi wa jimbo husika au mwombaji anaweza kufanya maombi kwa njia ya kielektroniki;

(iii) mwombaji atawasilisha maombi na kuambatisha uthibitisho wa kuandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(iv) msimamizi wa uchaguzi, baada ya kupokea fomu za maombi ataziwasilisha Tume ndani ya siku mbili (2) baada ya tarehe ya mwisho ya kupokea maombi;

(v) kwa kuzingatia masharti ya Sheria na Kanuni za uchaguzi, Tume inaweza kukubali au kukataa maombi hayo;

(vi) endapo Tume imekubali maombi yaliyowasilishwa itahamisha taarifa za mpiga kura kutoka katika kituo alichojiandikisha kwenda katika kituo alichoomba kupigia kura: Isipokuwa kwamba, uhamisho wa taarifa za mpiga kura katika utaratibu huu utakuwa ni kwa ajili ya uchaguzi husika na sio uhamisho wa kudumu;

(vii) Tume, ndani ya siku nane (8) kabla ya siku ya uchaguzi, itatoa orodha ya wapiga kura ambao maombi yao yamekubaliwa na kuwasilisha kwa wasimamizi wa uchaguzi au mtu mwingine yeyote aliyeteuliwa na Tume ambaye atahakikisha orodha hiyo inabandikwa katika eneo linaloonekana kwa urahisi katika vituo vya kupigia kura;

(viii) ndani ya siku nane (8) kabla ya siku ya uchaguzi, Tume itamtaarifu mwombaji ambaye maombi yake yamekubaliwa kwa:-

(a) kumtumia ujumbe kupitia simu ya mkononi;

(b) kupitia wasimamizi wa uchaguzi wa eneo husika, kumpa taarifa baada ya mwombaji kufuatilia majibu ya maombi yake; au

(c) njia nyingine yoyote kadiri Tume itakavyoona inafaa.

(ix) Tume itapeleka taarifa za wapiga kura walioomba na kukubaliwa katika vituo walivyojiandikisha;

(x) Tume inaweza kuvipatia vyama vya siasa nakala tepe ya orodha ya wapiga kura waliokubaliwa kupiga kura katika vituo tofauti na vituo walivyojiandikisha; na

(xi) wapiga kura walioruhusiwa kupiga kura ya Rais katika vituo vya kupigia kura tofauti na vituo walivyoandikishwa watachukuliwa kuwa ni wapiga kura walioandikishwa katika Daftari la kituo walichoruhusiwa kupiga kura kwa madhumuni ya uchaguzi husika pekee.

## 5.6 Uratibu, Usimamizi na Uendeshaji wa Uchaguzi katika Magereza na Vyuo vya Mafunzo

Kwa mujibu wa kanuni ya 45 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, kutakuwa na vituo vya kupigia kura kwenye magereza kwa Tanzania Bara na vyuo vya mafunzo kwa Tanzania Zanzibar.

### 5.6.1 Watendaji wa uchaguzi

(i) Tume kwa kushauriana na Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo, itateua waratibu wa uchaguzi kutoka miongoni mwa maafisa magereza au vyuo vya mafunzo kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwa na ufanisi wa utendaji katika vituo vya kupigia kura.

(ii) Waratibu wa uchaguzi katika magereza au vyuo vya mafunzo watakuwa wawili mmoja atashughulikia uratibu wa magereza kwa upande wa Tanzania Bara na mwingine vyuo vya mafunzo kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

(iii) Kituo cha kupigia kura katika gereza na chuo cha mafunzo kitakuwa na afisa wa Tume atakayekuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria, Kanuni, miongozo, maelekezo na taratibu za uchaguzi zinazingatiwa.

(iv) Kituo cha kupigia kura ndani ya gereza na chuo cha mafunzo kitakuwa na msimamizi wa kituo, msimamizi msaidizi wa kituo na karani mwongozaji watakaoteuliwa na msimamizi wa uchaguzi katika jimbo husika baada ya kufanya mashauriano na Tume pamoja na Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo.

### 5.6.2 Majukumu ya watendaji wa uchaguzi katika vituo vya kupigia kura ndani ya magereza na vyuo vya mafunzo

(i) Mratibu atakuwa na majukumu yafuatayo;

(a) kuratibu uendeshaji wa zoezi la uchaguzi katika vituo vya kupigia kura katika magereza na vyuo vya mafunzo;

(b) kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya uchaguzi na rasilimali nyingine;

(c) kuratibu taarifa zinazohusiana na uchaguzi;

(d) kuratibu masuala yote muhimu kwa ajili ya kuendesha uchaguzi kwa ufanisi katika vituo vya kupigia kura katika magereza na vyuo vya mafunzo; na

(e) kuchukua hatua nyingine muhimu ili kufanikisha uchaguzi.

(ii) Majukumu ya watendaji wa vituo vya kupigia kura ndani ya magereza na vyuo vya mafunzo ni kama yalivyoainishwa kwenye Sheria na Kanuni;

(iii) Watendaji wanaoshughulikia vituo vya kupigia kura vilivyopo ndani ya magereza na vyuo vya mafunzo watatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia masharti ya Sheria na Kanuni, ikiwa ni pamoja na kutoa tamko la kujitoa uanachama au kutokuwa mwanachama wa chama cha siasa na kuapa kiapo cha kutunza siri; na

(iv) Watendaji wa vituo vya kupigia kura ndani ya magereza watawajibika kwa msimamizi wa uchaguzi katika jimbo husika.

### 5.6.3 Watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura kilichopo ndani ya gereza na chuo cha mafunzo

Watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura kilichopo ndani ya gereza na chuo cha mafunzo ni-

(i) msimamizi wa kituo;

(ii) msimamizi msaidizi wa kituo;

(iii) karani mwongozaji;

(iv) mpiga kura ambaye ni mfungwa, mwanafunzi wa chuo cha mafunzo au mahabusu;

(v) msimamizi wa uchaguzi;

(vi) msimamizi msaidizi wa uchaguzi aliyeidhinishwa;

(vii) mratibu wa uchaguzi katika magereza na vyuo vya mafunzo;

(viii) Mjumbe wa Tume;

(ix) Mkurugenzi wa Uchaguzi; na (x) afisa wa Tume.

**5.6.4 Wafungwa, wanafunzi wa vyuo vya mafunzo na mahabusu wanaoruhusiwa kupiga kura na aina ya kura watakayopiga**

(i) Wafungwa, wanafunzi wa vyuo vya mafunzo na mahabusu watakaopiga kura ni;-

a) walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika vituo vya kupigia kura vilivyopo ndani ya magereza na vyuo vya mafunzo husika;

b) walioandikishwa kabla ya kuhukumiwa kutumikia kifungo kisichozidi miezi sita (6) gerezani au chuo cha mafunzo na kupata kibali cha Tume cha kupiga kura ya Rais katika vituo vya kupigia kura tofauti na vituo walivyojiandikisha; na

c) waliohamishwa gereza au chuo cha mafunzo na kupata kibali cha Tume cha kupiga kura ya Rais katika vituo vya kupigia kura tofauti na vituo walivyojiandikisha.

(ii) Kura itakayopigwa ni ya Rais tu.

**5.6.5 Utaratibu wa kuingia katika vituo vya kupigia kura vilivyopo katika magereza na vyuo vya mafunzo**

(i) Tume, baada ya kushauriana na Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo, itaweka utaratibu maalumu wa kuwawezesha watendaji wa vituo vya kupigia kura ndani ya gereza na chuo cha mafunzo au watendaji wengine wa uchaguzi ambao siyo maafisa magereza kuingia katika vituo vilivyopo gerezani na chuo cha mafunzo kutekeleza majukumu yao.

(ii) Watendaji wa vituo vya kupigia kura na watendaji wengine wa uchaguzi watakaoingia katika vituo vya kupigia kura vilivyopo

katika magereza na katika vyuo vya mafunzo, watapewa utambulisho maalumu ambao watapaswa kuwa nao muda wote wa utekelezaji wa majukumu yao.

### 5.6.6 Mashauriano kati ya Tume, jeshi la magereza na chuo cha mafunzo

Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa utaratibu wa kupiga kura kwa wafungwa, wanafunzi wa vyuo vya mafunzo na mahabusu, kutakuwa na mashauriano ya mara kwa mara kati ya Tume, Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo. Aidha, bila kuathiri sheria na kanuni zinazosimamia Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo, masharti ya Sheria, Kanuni na taratibu za uchaguzi zilizopo pamoja na maelekezo yatakayotolewa na Tume yatazingatiwa katika mchakato wa uchaguzi.

## 5.7 Fomu na Vifaa vya Kupigia Kura

Fomu na vifaa vitakavyotumika siku ya uchaguzi vitatakiwa kugawanywa kwa kuzingatia mahitaji halisi ya vituo. Msimamizi wa uchaguzi anatakiwa kuhakikisha zoezi la upangaji wa vifaa linakamilika kabla ya mafunzo ya watendaji wa vituo ili baada ya mafunzo avigawe kwa wasimamizi wa vituo.

**Fomu na Vifaa vitakavyotumika siku ya kupiga kura**

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| 1. | Masanduku ya kura. Sanduku la kura la kila uchaguzi litakuwa na mfuniko wenye rangi tofauti kama ifuatavyo: | Hutumika kutumbukiza karatasi za kura baada ya mpiga kura kupiga kura yake. |

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| | - Bluu kwa uchaguzi wa Rais<br>- Nyeusi kwa uchaguzi wa Mbunge<br>- Nyeupe kwa uchaguzi wa Diwani. | |
| 2. | Karatasi za kura. | Hutumika kwa ajili ya kura ya Rais, Mbunge na Diwani. |
| 3. | Muhuri wa kituo | Hutumika kugonga karatasi ya kura kabla mpiga kura hajakabidhiwa kwenda kwenye kituturi. Pia hutumika kugonga vibali vya watendaji au mawakala (fomu na. 18) na vibali vya wagombea (fomu na. 19) na fomu nyingine kama itakavyoelekezwa na Tume. |
| 4. | Wino maalumu usiofutika (*Indelible ink).* | Hutumika kwa wapiga kura kupakwa katika kidole cha mwisho cha mkono wa kushoto, baada ya kupiga kura na kabla ya kuondoka kituoni. |
| 5. | Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. | Hutumika kuthibitisha wapiga kura wanaostahili kupiga kura katika kituo husika. |
| 6. | **Fomu Na. 13** – Hesabu ya Karatasi za Kura. | Ni fomu ya kujaza idadi ya karatasi za kura zilizopokelewa na namba zake ambazo hujazwa kabla ya kuanza kupiga kura. Vilevile, hutumika kujaza idadi ya karatasi za kura zilizotumika, zilizoharibika na zisizotumika baada ya kukamilika kupiga kura kituoni. |

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| 7. | **Fomu za Malalamiko:**<br>**Fomu Na. 14** Kuridhika au kutoridhika kwa wakala wa upigaji kura kabla ya kuanza kupiga kura na baada ya kupiga kura. | Hujazwa na mawakala wa upigaji kura kabla ya kuanza kupiga kura na baada ya kukamilika kupiga kura kuonyesha kuridhika au kutoridhika na mwenendo wa kupiga kura kituoni. |
| | **Fomu Na. 15** Malalamiko ya mpiga kura kuhusu mwenendo wa kupiga kura katika kituo cha kupigia kura. | Hujazwa na mpiga kura ambaye ana malalamiko juu ya mwenendo wa kupiga kura au juu ya utendaji wa msimamizi wa kituo au msimamizi msaidizi wa kituo. |
| | **Fomu Na. 16** Kuridhika au kutoridhika kwa mgombea au wakala katika hatua ya kuhesabu kura. | Hujazwa na wakala au mgombea katika hatua za kuhesabu kura kuonesha kuridhika au kutoridhika na mwenendo wa kuhesabu kura kwa mujibu wa sheria. |
| 8. | **Fomu Na. 17** Tamko la mpiga kura | Tamko hili hutolewa na mpiga kura aliyetiliwa shaka na msimamizi wa kituo au wakala kuwa amekwisha piga kura au hana haki ya kupiga kura. |
| 9 | **Fomu Na. 18** Kibali cha kumwezesha mtendaji wa uchaguzi au wakala wa upigaji kura kupiga kura katika kituo ambacho hakujiandikisha. | Hutumika kumruhusu mtendaji wa uchaguzi aliyeainishwa kwa mujibu wa sheria na wakala wa upigaji kura kupiga kura katika kituo ambacho hakujiandikisha katika jimbo au kata husika. |

| | | |
|---|---|---|
| 10. | **Fomu Na. 19** Kibali cha | Hutumika kumwezesha mgombea |

| Na. | Aina ya Kifaa | Matumizi |
|---|---|---|
| | kumwezesha mgombea kupiga kura sehemu ambayo hakujiandikisha ndani ya eneo la uchaguzi alilojiandikisha. | kupiga kura katika kituo ambacho hakujiandikisha ndani ya eneo la uchaguzi alilojiandikisha. |
| 11. | **Fomu Na. 20** Taarifa ya msimamizi wa kituo cha kupigia kura. | Hutumiwa na msimamizi wa kituo kujaza taarifa mbalimbali baada ya kufunga kituo. |
| 12. | Seti ya lakiri (*seals*) za plastiki za kufungia masanduku | Hutumika kufungia masanduku ya kura kabla ya kuanza kupiga kura, wakati wa kufunga kituo na baada ya kumaliza zoezi la kuhesabu kura. |
| 13. | Kalamu za wino. | Hutumika kuandikia na kuweka alama ya vema **(√)** katika karatasi ya kura. |
| 14. | Jalada la nukta nundu "*Tactile Ballot folder*" kwa ajili ya watu wasioona. | Ni kifaa kinachotumika kuwawezesha watu wasioona kupiga kura wenyewe kwa kutumia alama za nukta nundu |
| 15. | Vituturi (*Polling Booths*). | Hutumika kuwawezesha wapiga kura kupiga kura kwa siri kwa mujibu wa sheria. kwa wale wenye ulemavu wasioweza kutumia kituturi cha kawaida, kituturi kigeuzwe chini-juu (*upside-down*) ili kiwe kifupi. hii itawawezesha kupiga kura kwa urahisi. |

| | | |
|---|---|---|
| 16. | Orodha ya majina ya wapiga kura (Nakala 2). | Hubandikwa nje ya kituo kuonesha majina ya wapiga kura wa kituo hicho. Nakala moja hutumiwa na karani mwongozaji wapiga kura kwa kuwasaidia wapiga kura kufahamu mahali |
| **Na.** | **Aina ya Kifaa** | **Matumizi** |
| | | walipopangiwa kupiga kura zao. |
| 17. | Vitabu vya Fomu za Matokeo: 21A, 21B, 21C SEHEMU A na SEHEMU B. | Hutumika kujaza taarifa za matokeo katika kituo cha kupigia kura kwa kila aina ya uchaguzi.<br>**Fomu 21A:** Matokeo ya Rais.<br>**Fomu 21B:** Matokeo ya Mbunge.<br>**Fomu 21C:** Matokeo ya Diwani. SEHEMU A ya fomu husika hutumika kujaza matokeo ya kila mgombea kituoni. SEHEMU B ya fomu husika hutumika kujaza kura zenye mgogoro. |

### 5.8 Maandalizi Kabla ya Kupiga Kura Kituoni

(i) msimamizi wa kituo cha kupigia kura mara atakapowasili katika kituo, atakagua mazingira ya kituo ili kuhakikisha kuwa hakuna matangazo ya kampeni ya mgombea yeyote. Baada ya hapo anatakiwa kubandika bango la kituo cha kupigia kura, maelekezo na hadhari kwa mpiga kura na mfano wa karatasi ya kura;

(ii) msimamizi wa kituo anatakiwa kuwaonesha mawakala wa kupiga kura na mtu yeyote atakayekuwepo katika kituo cha kupigia kura kwamba sanduku la kura ni tupu, ili waweze kuhakikisha kuwa halina kitu chochote ndani yake;

(iii) kabla ya kuanza kupiga kura, msimamizi wa kituo hutakiwa kuwapa mawakala wa upigaji kura (kama wapo) Fomu na. 14 waijaze ili kutoa maoni kama wanaridhika au hawaridhiki na matayarisho ya kituo cha kupigia kura; na

(iv) muda wa kufungua kituo ukifika, msimamizi wa kituo hutakiwa kufungua kituo na kuwaruhusu watu wapige kura hata kama mawakala hawajafika.

### 5.8.1 Utaratibu wa kupiga kura

(i) mpiga kura atatakiwa kwenda na kadi yake ya kupigia kura kituoni na kumpa msimamizi msaidizi na. 1 wa kituo;

(ii) msimamizi msaidizi na. 1 atasoma jina la mpiga kura kwa sauti ili kuwawezesha mawakala kuangalia taarifa za mpiga kura huyo katika Daftari la kituo;

(iii) msimamizi msaidizi na. 1 ana haki ya kumuuliza mpiga kura swali lolote linalohusiana na utambulisho wake iwapo ana shaka naye;

(iv) msimamizi wa kituo kabla ya kumkabidhi mpiga kura karatasi za kura atagonga muhuri wa kituo;

(v) msimamizi wa kituo atampatia mpiga kura karatasi ya kupigia kura na kumuelekeza namna ya kuikunja karatasi hiyo baada ya kupiga kura;

(vi) mpiga kura atatakiwa kwenda katika kituturi na kupiga kura yake kwa siri;

(vii) mpiga kura atatakiwa kuweka alama ya vema (√) katika eneo la mgombea ambaye anamtaka katika karatasi ya kupigia kura;

(viii) mara baada ya kupiga kura, mpiga kura ataikunja karatasi yake ya kura na kuitumbukiza katika sanduku la kura lililowekwa katika eneo la wazi la kituo; na

(ix) kabla mpiga kura hajaondoka kituoni msimamizi msaidizi na. 2 atampaka wino maalumu kwenye kidole kidogo cha mwisho cha mkono wa kushoto.

### 5.8.2 Kuharibika kwa kura

Karatasi ya kura haitahesabiwa kuwa kura halali iwapo kura hiyo:-

(i) haina muhuri wa kituo;

(ii) imepigwa kwa mgombea zaidi ya mmoja;

(iii) ina alama, au maandishi yanayoweza kumtambulisha mtu aliyepiga kura;

(iv) haina alama yoyote; na

(v) amepigiwa mgombea aliyejitoa.

**5.8.3 Watu wanaoruhusiwa kuingia kwenye kituo cha kupigia kura** Kwa mujibu wa kifungu cha 85 (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024, wafuatao ndio wanaoruhusiwa kuingia kwenye Kituo cha Kupigia Kura:-

(i) msimamizi wa kituo cha kupigia kura;

(ii) wasimamizi wasaidizi wa kituo cha kupigia kura;

(iii) mawakala wa upigaji kura;

(iv) wapiga kura kwa ajili ya kupiga kura tu;

(v) mtu anayemsaidia mpiga kura asiyeweza kupiga kura mwenyewe;

(vi) mwangalizi aliyeidhinishwa na Tume kwa maandishi;

(vii) wagombea;

(viii) Mjumbe wa Tume;

(ix) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(x) afisa wa Tume;

(xi) afisa wa polisi au mtu anayehusika na usalama katika kituo cha kupigia kura;

(xii) msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi;

(xiii) mratibu wa uchaguzi wa mkoa; na (xiv) afisa uchaguzi.

Aidha, waandishi wa habari wanaweza kuruhusiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura kwa maelekezo yatakayotolewa na Tume.

**5.9 Kuhesabu Kura**

Kwa mujibu wa kifungu cha 92(1), (2) na (3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kura zitahesabiwa katika vituo vya kupigia kura. Mara baada ya kufunga kituo cha kupigia kura, kituo hicho

kitageuka kuwa kituo cha kuhesabia kura. Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi au msimamizi wa uchaguzi anaweza, kwa sababu za kiusalama, ufinyu wa nafasi ya kuhesabia au huduma nyingine au kwa sababu nyingine za msingi, kuelekeza kuwa kura za vituo kadhaa vya kupigia kura vilivyo karibu au vituo vyote vya kupigia kura katika eneo la uchaguzi au mchanganyiko wa maeneo ya uchaguzi yaliyo jirani, zitahesabiwa katika sehemu moja. Katika kuhesabu kura itahakikishwa kwamba kura zitakazohesabiwa hazitachanganywa na hesabu ya kura za vituo vingine.

### 5.9.1 Watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kuhesabia kura ni:

(i) msimamizi wa kituo;

(ii) msimamizi msaidizi wa kituo;

(iii) mgombea kama atakuwepo;

(iv) wakala wa upigaji kura;

(v) mwangalizi aliyeidhinishwa na Tume kwa maandishi;

(vi) Mjumbe wa Tume;

(vii) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(viii) afisa wa Tume;

(ix) mratibu wa uchaguzi wa mkoa;

(x) msimamizi wa uchaguzi;

(xi) msimamizi msaidizi wa uchaguzi; na

(xii) askari polisi au mtu anayehusika na usalama wa mahali pa kuhesabia kura.

### 5.9.2 Utaratibu wa kufuata wakati wa kuhesabu kura

Kwa mujibu wa kifungu cha 95 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kabla ya kuanza kujumlisha kura, wahusika watazingatia yafuatayo:-

(i) watahakiki na kuandika idadi ya watu wote waliopiga kura katika kituo cha kupigia kura;

(ii) watahesabu na kuandika idadi na karatasi za kura zote ambazo hazikutumika, zikijumuisha karatasi za kura zote zilizoharibika na kuzifunga katika bahasha maalumu;

(iii) watakagua lakiri na kuhakikisha kama imefunguliwa;

(iv) watafungua lakiri;

(v) watafungua sanduku la kura;

(vi) mgombea au wakala wa kuhesabu kura, ikiwa ameridhika au hajaridhika wakati wa kukagua masanduku, kuthibitisha idadi ya kura zilizomo ndani ya kila sanduku au kuhesabu kura alizopata kila mgombea atajaza Fomu Na. 16.

#### 5.9.3 Kura zitakazohesabiwa kuwa zimekataliwa

Kwa mujibu wa kifungu cha 96(1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, karatasi ya kura itachukuliwa kuwa imekataliwa iwapo:- (i) haina alama rasmi;

(ii) haina muhuri wa kituo;

(iii) itakuwa na kitu au alama yoyote yenye kumtambulisha mpiga kura;

(iv) kura yoyote itakayopigwa kwa mgombea aliyejitoa kwa mujibu wa sheria za uchaguzi;

(v) alama imewekwa kwa mgombea zaidi ya mmoja; na (vi) haina alama yoyote.

#### 5.9.4 Uamuzi wa kura kuwa halali au kutokuwa halali

Kwa kuzingatia kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi, kadiri itakavyokuwa, ataamua uhalali wa kura zenye mgogoro kabla ya kuanza kujumlisha kura na kuandika matokeo katika Sehemu B ya Fomu Na. 21A, 21B au 21C mtawalia, ikionesha idadi ya kura zenye mgogoro alizopata kila mgombea na kuagiza fomu hizo kusainiwa na wagombea au mawakala wa upigaji kura, ikiwa wapo.

#### 5.9.5 Kura zenye mgogoro, kura zilizokataliwa na kura halali

(i) Kura zenye mgogoro

Kura yenye mgogoro inatokea iwapo mawakala wa kuhesabu kura au mgombea wa chama kushindwa kufikia muafaka kuhusu uhalali wa kura husika. Iwapo kutatokea kuwepo kwa kura zenye mgogoro, zitawekwa kwa utaratibu ufuataao:-

(i) kura za kiti cha Rais zenye mgogoro zitawekwa kwenye Bahasha Na. 5A;

(ii) kura za ubunge zenye mgogoro zitawekwa kwenye Bahasha Na. 5B; na

(iii) kura za udiwani zenye mgogoro zitawekwa kwenye Bahasha Na. 5C.

(ii) Kura zilizokataliwa

Iwapo kutakuwa na kura zilizokataliwa, zitawekwa kwa utaratibu ufuataao:-

(i) kura za kiti cha Rais zilizokataliwa zitawekwa kwenye Bahasha Na. 6A;

(ii) kura za ubunge zilizokataliwa zitawekwa kwenye Bahasha Na. 6B; na

(iii) kura za udiwani zilizokataliwa zitawekwa kwenye Bahasha Na. 6C.

(iii) Kura halali

Kura halali zitawekwa kwa utaratibu ufuataao:-

(i) kura halali za kiti cha Rais zitawekwa kwenye Bahasha Na. 7A;

(ii) kura halali za ubunge zitawekwa kwenye Bahasha Na. 7B; na

(iii) kura halali za udiwani zitawekwa kwenye Bahasha Na. 7C.

### 5.10 Taarifa ya Majumuisho ya Kura

Kwa mujibu wa kanuni ya 53 ya Kanuni za uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi kabla ya kuanza kupokea fomu za matokeo na vifaa kutoka

katika vituo vyote vya kupigia kura katika jimbo au kata, atavitaarifu vyama vya siasa au wagombea tarehe, muda na mahali pa kujumlishia kura.

### 5.10.1 Watu wanaoruhusiwa kuingia katika chumba cha kujumlisha kura

Kwa mujibu wa kifungu cha 103 (2) cha cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, watu wafuatao wanaruhusiwa kuwepo katika kituo cha kujumlisha kura:-

(i) msimamizi wa uchaguzi;

(ii) msimamizi msaidizi wa uchaguzi;

(iii) mratibu wa uchaguzi wa mkoa;

(iv) Mjumbe wa Tume;

(v) Mkurugenzi wa uchaguzi;

(vi) afisa wa Tume;

(vii) mgombea;

(viii) wakala wa kuhesabu kura;

(ix) afisa wa polisi au mtu anayehusika na usalama mahali pa kuhesabia kura;

(x) mwangalizi aliyeidhinishwa na Tume kwa maandishi; na (xi) afisa uchaguzi.

### 5.10.2 Utaratibu wa kufuata kabla ya kuanza kujumlisha kura

Kabla ya kuanza kujumlisha kura, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atatoa maelezo kuhusu utaratibu utakaofuatwa na maadili ambayo waliomo katika chumba cha kujumlisha kura watapaswa kuyafuata;

(i) msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atatoa taarifa kuhusu matukio muhimu ambayo ana habari nayo, kuhusu mwenendo wa uchaguzi kwa ujumla;

(ii) msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi awape wagombea nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu mwenendo wa uchaguzi; na

(iii) msimamizi wa uchaguzi anatakiwa aanze kujumlisha kwanza matokeo ya uchaguzi wa Rais ili yaweze kutumwa Tume mapema.

### 5.10.3 Utaratibu wa kufuata wakati wa kujumlisha kura

(i) msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atahahakisha kwamba masanduku ya kura yote na Fomu Na. 21A, 21B na 21C Sehemu A na Sehemu B vimepokelewa;

(ii) msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi anaruhusiwa kufungua bahasha zifuatazo kwenye chumba cha kujumlishia kura;- (a) Bahasha ya kituo;

(b) Bahasha Na. 1 (Hesabu ya Karatasi za Kura);

(c) Bahasha Na. 3A, 3B, 3C (Karatasi za Kura ambazo hazikutumiwa na zilizoharibika); na

(d) Bahasha Na. 5A, 5B, 5C (Kura zenye Mgogoro).

(iii) baada ya kura zenye mgogoro kufanyiwa uamuzi na msimamizi wa uchaguzi, kura halali na kura zilizokataliwa zitaingizwa kwenye bahasha zinazohusika.

### 5.10.4 Kufungana kwa kura

Kwa mujibu wa kifungu cha 99 (1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, pale ambapo kutakuwa na wagombea waliopata idadi ya kura inayolingana na ikashindikana kupata mshindi baada ya kujumlisha kura zote, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi anatakiwa kufungua masanduku yote ya kura katika jimbo au kata na kuhesabu kura upya. Baada ya kuhesabu kura zote upya na kura kulingana tena atatakiwa kuitaarifu Tume. Tume itapanga siku nyingine ya uchaguzi ambayo haitakuwa zaidi ya siku thelathini (30) tangu siku ya uchaguzi wa awali. Wakati upigaji kura utakaporudiwa, watakaopigiwa kura ni wale tu ambao katika uchaguzi wa awali walipata kura nyingi kuliko wagombea wengine na kura zao zililingana.

### 5.10.5 Ombi la kurudia kuhesabu kura

Msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atalikubali ombi la kurudia kuhesabu kura za wagombea kwa kituo ikiwa usahihi wa kura za kituo au vituo husika ulipingwa na wakala au mgombea katika kituo cha kuhesabia kura. Baada ya kukamilisha zoezi hilo, msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi atajumlisha kura alizopata kila mgombea.

### 5.10.6 Matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais

Msimamizi wa uchaguzi, mara baada ya kujumlisha kura za uchaguzi wa Rais:-

(i) atajaza Fomu Na. 22A inayoonesha matokeo ya uchaguzi wa Rais kwa kila kituo cha kupigia kura katika jimbo;

(ii) atajaza Fomu Na. 23A inayoonesha matokeo ya uchaguzi wa Rais kwa kila chama cha siasa kwenye kila kituo cha kupigia kura katika jimbo;

(iii) atajaza Fomu Na. 24A inayoonesha matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais katika jimbo husika;

(iv) atatoa kwa kila mgombea au wakala wake, ikiwa yupo, nakala ya Fomu Na. 24A ya matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais;

(v) atabandika nakala ya Fomu Na. 24A katika ubao wa matangazo kwenye ofisi ya msimamizi wa uchaguzi ya jimbo husika; na

(vi) atawasilisha mara moja kwa Tume matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais katika jimbo hilo kupitia Fomu Na. 24A.

### 5.10.7 Matokeo ya uchaguzi wa Rais

Tume, kabla ya kupokea matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais kutoka majimbo yote ya uchaguzi, itavijulisha vyama vya siasa au wagombea wanaohusika kuhusu tarehe, muda na mahali pa kufanya majumuisho ya kura.

Baada ya kupokea matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais yaliyowasilishwa chini ya kanuni ya 54 na baada ya kuyathibitisha, Tume itatangaza matokeo ya awali ya uchaguzi wa Rais kwa jimbo husika. Tume itajumlisha matokeo yote ya awali ya uchaguzi wa Rais kwa kila mgombea yaliyowasilishwa kwake na wasimamizi wa uchaguzi na:-

(i) itajaza Fomu Na. 25 inayoonesha matokeo ya uchaguzi wa Rais kwa kila jimbo; na

(ii) itajaza Fomu Na. 26 inayoonesha matokeo ya uchaguzi wa Rais kwa kila chama cha siasa kwenye kila jimbo.

Baada ya kujumlisha matokeo ya awali ya kila jimbo, Tume: -

(i) itajaza matokeo ya uchaguzi wa Rais kwenye Fomu Na. 27;

(ii) itawataka wagombea au mawakala ikiwa wapo, kusaini Fomu Na. 27;

(iii) itamtangaza mgombea ambaye amepata kura halali nyingi zaidi kuliko mgombea mwingine yeyote kuwa Rais aliyechaguliwa;

(iv) itampa kila mgombea au wakala wake nakala ya Fomu Na. 27; na

(v) itabandika nakala ya Fomu Na. 27 katika ubao wa matangazo wa ofisi za Tume.

Tume, mara baada ya kutangaza matokeo, itatoa kwa mgombea aliyechaguliwa, hati ya kuchaguliwa kuwa Rais na hati ya kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilizoainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 ikionesha–

(i) jina kamili la mgombea aliyechaguliwa;

(ii) chama cha siasa cha mgombea aliyechaguliwa;

(iii) tarehe ya uchaguzi na tarehe ya kutolewa hati;

(iv) wadhifa aliopata mgombea aliyechaguliwa; na

(v) saini ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Tume.

### 5.11 Wakala wa Upigaji Kura

Kwa kuzingatia kifungu cha 77(1)(2) na 91(1)(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kila chama cha siasa kinaweza, baada ya kupata ridhaa ya wagombea, kuteua mtu mmoja atakayejulikana kama wakala wa upigaji kura au wakala wa kuhesabu kura kwa kila kituo ndani ya jimbo au kata ambayo ina mgombea. Vilevile, wakala wa upigaji kura, wakati wa kuhesabu kura, atakuwa wakala wa kuhesabu kura.

Orodha ya mawakala walioteuliwa na chama husika itawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi kwa maandishi siku saba (7) kabla ya siku ya uchaguzi au ndani ya muda mfupi zaidi kama itakavyoelekezwa na Tume. Orodha hiyo itataja jina na anwani ya kituo cha kupigia kura ambacho wakala amepangiwa.

Chama cha siasa kinaweza kuteua wakala mbadala wa upigaji kura, ambaye anaweza kuwepo na kutekeleza majukumu yoyote ya wakala wa upigaji kura pale ambapo wakala wa upigaji kura anayehusika hatakuwepo katika kituo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kufariki. Aidha, mawakala wa upigaji kura hawataruhusiwa kuwepo katika vituo vya kupigia kura vilivyopo ndani ya magereza na vyuo vya mafunzo.

#### 5.11.1 Majukumu ya wakala wa upigaji kura

Majukumu ya wakala wa upigaji kura ni yafuatayo:-

(i) kuwabaini watu wanaostahili kupiga kura;

(ii) kumwakilisha na kulinda maslahi ya mgombea au wagombea katika kituo cha kupigia kura; na

(iii) kushirikiana na msimamizi wa kituo na wasimamizi wasaidizi wa kituo ili kuhakikisha sheria na taratibu zinazohusu upigaji kura na chaguzi zinazingatiwa katika kituo.

### 5.11.2 Sifa za wakala wa upigaji kura

Ili mtu aweze kuwa wakala wa upigaji kura kwenye uchaguzi, atahitajika kuwa na sifa zifuatazo:-

(i) awe na miaka kumi na nane (18) na kuendelea;

(ii) awe na akili timamu;

(iii) awe ameteuliwa na chama chake cha siasa;

(iv) awe ameidhinishwa na msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi; na

(v) awe ameapa kiapo cha kutunza siri kwa kutumia Fomu Na. 7.

Inashauriwa wakala awe ni mkazi wa eneo la kituo anachokisimamia, hii itamsaidia wakala kushiriki pia katika uchaguzi wa ngazi zote tatu za urais, ubunge na udiwani.

### 5.11.3 Wakala wa upigaji kura au mgombea kuridhika au kutoridhika katika kituo cha kupigia kura

Kwa mujibu wa kanuni ya 44 na 51 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 wakala au mgombea atajaza fomu zifuatazo:-

(i) **Fomu Na. 14:** Hii ni fomu ya kuridhika au kutoridhika kwa wakala wa kupiga kura. Fomu hii hujazwa na wakala kabla ya kuanza na baada ya kukamilika kupiga kura kuonesha kuridhika au kutokuridhika na mwenendo wa kupiga kura**.**

(ii) **Fomu Na. 16:** Hii ni fomu ya kuridhika au kutoridhika kwa mgombea au wakala wa kuhesabu kura. Fomu hii hujazwa na Wakala katika hatua za kuhesabu kura kuonesha kuridhika au kutoridhika na utaratibu wa kuhesabu kura.

#### 5.11.4 Utambulisho wa mawakala wa upigaji kura

Kwa mujibu wa kanuni ya 40 (8) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2025, barua ya utambulisho wa kila wakala itakayowasilishwa na chama iainishe kituo alichopangiwa na iambatishwe picha mbili za rangi zenye ukubwa sawa na picha inayotumika katika pasi ya kusafiria (*passport size*) zilizopigwa si zaidi ya miezi mitatu (3), kitambulisho cha taifa, kadi ya mpiga kura au pasi ya kusafiria.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 77(2) na (3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024, chama kitaruhusiwa kuteua wakala mbadala endapo aliyeteuliwa awali amefariki au ameshindwa kutekeleza majukumu ya uwakala. Katika kurahisisha utekelezaji wa suala hili, sambamba na orodha ya mawakala wa vituoni, vyama vinaweza kuwasilisha majina mawili (2) ya mawakala wa ziada kwa kila kata ambao watatumika kama mawakala wa upigaji kura mbadala iwapo watahitajika. Ikumbukwe kuwa kutokuwepo kwa wakala wa chama chochote kinachoshiriki uchaguzi katika kituo cha kupigia kura, kuhesabu au kujumlisha matokeo ya kura hakutasimamisha, kuchelewesha au kubatilisha mchakato wa uchaguzi.

**Maswali ya tafakuri**

1. Taja sifa za mtu kuweza kupiga kura.
2. Je, kura itahesabika kutokuwa halali au kuharibika iwapo nini kimetokea?
3. Je, mwananchi anawezaje kujua kituo chake cha kupigia kura?
4. Nani anaruhusiwa kuingia katika Kituo cha kupigia na kuhesabu kura?
5. Je, ikiwa wakala hatakuwepo katika kituo cha kuhesabia kura, zoezi linaweza kuathirika?
6. Je, ikiwa idadi ya kura za wagombea zimelingana nini kitafanyika?
7. Taja majukumu ya wakala katika kituo cha kupigia kura.

# SURA YA SITA

# WABUNGE NA MADIWANI WANAWAKE WA VITI MAALUMU

## 6.0 Utangulizi

Sura hii inaeleza utaratibu unaotumika kuwapata wabunge na madiwani wanawake wa viti maalumu kwa kila chama kilichoshiriki uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani.

## 6.1 Malengo ya Sura ya Sita

Kumwezesha mwananchi kuelewa mambo yafuatayo:- (i)

Uteuzi wa viti maalumu.

(ii) Utaratibu wa upatikanaji wa orodha ya wanaopendekezwa kuteuliwa kuwa wabunge na madiwani wanawake viti maalumu.

(iii) Ukokotoaji wa kupata viti maalumu.

**Mambo Muhimu katika sura hii**

- **Bunge;**
- **Baraza la halmashauri; na**
- **Wabunge na madiwani wanawake viti maalumu.**

## 6.2 Viti Maalumu

Wabunge na madiwani wanawake wa viti maalumu hupatikana mara baada ya kukamilika zoezi la kupiga kura na utangazaji wa matokeo ya urais. Hii ni baada ya idadi ya kura zote halali kupatikana, ambazo husaidia ukokotoaji wa idadi ya wabunge wanawake wa viti maalumu wanaohitajika. Ibara ya 66(1)(b) na 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kifungu cha 112 na 113 cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, kwa pamoja vinaanzisha utaratibu wa kuwepo na namna ya kuwapata wabunge na madiwani wanawake wa viti maalumu.

## 6.3 Utaratibu wa Kuwapata Wabunge na Madiwani Wanawake wa Viti

**Maalumu**

(i) chama cha siasa kinachogombea katika uchaguzi wa ubunge na udiwani utakaofanyika baada ya kuvunjwa kwa Bunge, kinaweza kupendekeza majina ya wagombea wanawake wenye sifa kwa uteuzi wa viti maalumu kwa wanawake wa ubunge na udiwani na kuituma orodha ya majina hayo Tume siku thelathini (30) kabla ya uchaguzi;

(ii) chama cha siasa kitahakikisha kwamba wanawake wanaopendekezwa kuteuliwa kuwa wabunge na madiwani wa viti maalumu wanajaza fomu za uteuzi (Fomu Na. 8D kwa wabunge wanawake wa viti maalumu na Fomu Na. 8E kwa madiwani wanawake wa viti maalumu) na kuziwasilisha Tume pamoja na Picha nne (4) za ukubwa sawa na picha ya hati ya kusafiria (*passport size*) zenye muonekano wa rangi nyeupe nyuma (*white background*);

(iii) fomu hizo lazima zisainiwe na katibu wa mkoa au wilaya wa chama cha siasa, kula kiapo mbele ya hakimu, kusainiwa na kupigwa muhuri wa mahakama;

(iv) majina ya wanawake wagombea waliopendekezwa na vyama vya siasa kwa Tume yatakuwa katika mpangilio kwa kuzingatia kipaumbele;

(v) Tume itaainisha idadi ya wanawake wagombea waliopendekezwa kuteuliwa na kila chama cha siasa;

(vi) mwanamke aliyependekezwa ni lazima adhaminiwe na chama chake cha siasa;

(vii) Tume kwa kuzingatia Ibara 66 na 67 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kwa mujibu wa mpangilio kwa kuzingatia kipaumbele ulioainishwa katika orodha iliyopendekezwa na kila chama cha siasa, Tume itateua na kutangaza idadi ya wanawake wagombea kutoka katika vyama vya siasa husika kuwa wabunge na madiwani wa viti maalumu;

(viii) kwa wabunge wanawake wa viti maalumu, Tume itatuma taarifa ya uteuzi kwa Spika wa Bunge na kwa makatibu wakuu wa vyama

vya siasa husika. Aidha, kwa madiwani viti maalumu wanawake, Tume itatuma taarifa kwa halmashauri na kwa makatibu wakuu wa vyama vya siasa husika;

(ix) orodha ya majina ya wagombea wanawake waliopendekezwa na chama cha siasa kwa Tume kwa mujibu wa Ibara ya 78(4) na 76(3)ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na kila chama cha siasa kwa uchaguzi mkuu, itakuwa orodha sawa na ile itakayotumiwa na Tume kwa madhumuni ya kujaza nafasi yoyote iliyo wazi ya ubunge wa viti maalumu vya wanawake wakati wa kipindi kizima cha uhai wa Bunge na Baraza la Madiwani;

(x) wanawake watakaopendekezwa hawahitajiki kuweka dhamana; na

(xi) baada ya Tume kutuma taarifa ya tamko kwa Spika wa Bunge na kwa makatibu wakuu wa vyama vya siasa husika na kwa madiwani viti maalumu wanawake na taarifa kwa halmashauri na kwa makatibu wakuu wa vyama vya siasa husika, orodha ya majina hayo itachapishwa kwenye Gazeti la Serikali.

## 6.4 Wabunge Wanawake wa Viti Maalumu

Kwa mujibu wa Ibara ya 66(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, idadi ya wabunge wanawake wa viti maalumu haitapungua 30% ya Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya kisera ya Mwaka 2010 yaliyofanywa na Serikali idadi ya wabunge wanawake wa viti maalumu isipungue asilimia arobaini (40%) ya Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 6.4.1 Namna ya kupata asilimia 40 ya wabunge wanawake wa viti maalumu

Ili kujua wanawake wa viti maalumu ambao ni asilimia arobaini (40%) ya wabunge wote ni wangapi, kanuni ifuatayo hutumika:-

*Idadi ya Wabunge wa Majimbo 264 **unajumlisha** na Wabunge 5 kutoka Baraza la Wawakilishi, **unajumlisha** Wabunge 10 wa kuteuliwa na Rais, **unajumlisha** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, **unajumlisha** na Spika iwapo atakuwa si Mbunge halafu **unazidisha** kwa 40 na **unagawanya** kwa 100.*

***(Wabunge wa Jimbo + Wabunge 5 wa Baraza la Wawakilishi + Wabunge 10 wa kuteuliwa + Mwanasheria Mkuu wa Serikali + Spika iwapo siyo Mbunge) X 40 100***

### 6.4.2 Kupata asilimia tano (5%) ya kura zote za ubunge

Kwa mujibu wa Ibara ya 78(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kila chama cha siasa kilichoshiriki katika uchaguzi mkuu na kupata angalau asilimia tano (5%) ya kura zote halali za wabunge kitapata wabunge wa viti maalumu kulingana na kura ambazo chama husika kimepata.

*Idadi ya **Kura zote halali za ubunge** kwa vyama vyote vilivyoshiriki katika Uchaguzi Mkuu **unazidisha** kwa **tano** na **kugawanya** kwa **mia moja.***

***(Kura zote halali za ubunge za vyama vilivyoshiriki katika Uchaguzi Mkuu) X 5 =5%*** **100**

### 6.4.3 Kupata viti maalumu vya ubunge kwa kila chama

Kujumlisha idadi ya kura zote halali ambazo chama cha siasa kimepata kuzidisha na idadi ya viti maalumu vya ubunge na kugawanya kwa idadi ya kura zote halali za ubunge za vyama vilivyopata angalau asilimia tano (5%) ya kura zote halali za ubunge.

***Kura zote halali za ubunge ambazo Chama kimepata X Idadi ya viti maalumu vya ubunge***

***Idadi ya Kura zote halali za ubunge za vyama vyote vilivyopata angalau 5%***

### 6.5 Madiwani Wanawake Viti Maalumu

Kifungu cha 35(1)(d) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, kifungu cha 24(1)(c) cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 vinaainisha uwepo 1/3 ya viti maalumu vya udiwani kwenye kila halmashauri.

#### 6.5.1 Uteuzi wa madiwani wanawake wa viti maalumu

Tume baada ya kupokea orodha ya majina ya wanawake wanaopendekezwa kuteuliwa kuwa madiwani wanawake wa viti maalumu, vyama husika huteua madiwani hao kwa kila halmashauri kadiri ya idadi ambayo chama husika kinastahili kupata. Fomu Na. 8E hutumika kuomba Uteuzi wa kuwa diwani viti maalumu.

#### 6.5.2 Upatikanaji wa madiwani wa viti maalumu

Upatikanaji wa madiwani wanawake wa viti maalumu ni sawa na idadi ya kata zilizopo katika halmashauri husika, jumlisha na Mbunge au wabunge waliopo katika halmashauri hiyo unazidisha kwa moja na kugawanya kwa tatu.

$$\frac{(\text{Idadi ya kata katika halmashauri + mbunge au wabunge}) \times 1}{3}$$

#### 6.5.3 Upatikanaji wa idadi ya madiwani wa viti maalumu kwa kila chama

Ili kupata idadi ya madiwani kwa kila chama, unachukua idadi ya kata ambazo chama kimepata unazidisha na idadi ya viti maalumu katika halmashauri husika na kugawanya kwa idadi ya kata katika halmashauri husika.

$$\frac{\text{Idadi ya kata ambazo chama kimepata X Idadi ya viti maalumu katika halmashauri}}{\text{Idadi ya kata katika halmashauri}}$$

**Maswali ya tafakuri**

1. Ni nani anayeteua wabunge na madiwani wanawake viti maalumu?
2. Ni nani hupendekeza majina ya wabunge na madiwani wanawake viti maalumu?
3. Je, kila chama kilichosajiliwa kinastahili viti maalumu vya wanawake?
4. Je, uteuzi wa wabunge na madiwani wa viti maalumu hufanyika wakati gani?

## SURA YA SABA MAKOSA NA ADHABU WAKATI WA UCHAGUZI

### 7.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea makosa mbalimbali yanayohusu uchaguzi kuanzia hatua ya uteuzi hadi kutangazwa matokeo ya uchaguzi. Pia, inaelezea adhabu zitakazotolewa endapo watendaji wa uchaguzi na wadau wa uchaguzi watafanya makosa hayo.

### 7.1 Malengo ya Sura ya Saba

Kumwezesha mwananchi kuelewa:-

(i) makosa wakati wa uteuzi na uchaguzi; na

(ii) adhabu na faini kuhusu makosa ya uchaguzi.

**Mambo Muhimu katika Sura Hii**

- **makosa wakati wa uteuzi;**
- **makosa wakati wa uchaguzi; na**
- **adhabu zitakazotolewa dhidi ya makosa ya uteuzi na uchaguzi.**

### 7.2 Makosa na Adhabu

Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Na. 1 ya Mwaka 2024, imeainisha makosa mbalimbali yanayoweza kutendwa na watendaji wa uchaguzi, wadau wa uchaguzi pamoja na adhabu ya makosa hayo.

### 7.3 Makosa Yanayohusu Uteuzi na Uchaguzi

| Na. | Kosa | Kifungu cha Sheria | Adhabu |
|---|---|---|---|
| 1. | **Makosa ya Uteuzi**<br><br>Kutumia wadhifa kushawishi watu kuteuliwa au kujitoa katika ugombea. | **115** (1) | Faini isiyopungua Shilingi laki moja (100,000) za Kitanzania na isiyozidi<br>Shilingi laki tatu (300,000) za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu (3) na kisichozidi miezi kumi na |

| Na. | Kosa | Kifungu cha Sheria | Adhabu |
|---|---|---|---|
| | | | mbili (12) au vyote kwa pamoja. |
| 2. | **Makosa yanayohusu Fomu za Uteuzi au Karatasi za Kura**<br><br>(i) Anaghushi au kwa udanganyifu anafuta au anaharibu fomu ya uteuzi au karatasi ya kura au anawasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi fomu ya uteuzi akijua kuwa fomu hiyo imeghushiwa | 121(1)(a) | Faini isiyopungua Shilingi elfu hamsini (50,000) za Titanzania na isiyozidi laki tatu (300,000) za Kitanzania au kifungo kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miaka miwili (2) au vyote kwa pamoja. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (ii) anaghushi au anatengeneza au kwa udanganyifu anaharibu karatasi yoyote ya kura au alama rasmi katika karatasi yoyote ya kura. | 121(1)(b) | |
| | (iii) Msimamizi wa uchaguzi au msimamizi wa kituo kushindwa kuweka alama rasmi katika karatasi ya kura. | 121(1)(c) | |
| | (iv) Kusambaza karatasi za kura kwa mtu yeyote bila kuwa na mamlaka halali. | 121(1)(d) | |

| Na. | Kosa | Kifungu cha Sheria | Adhabu |
|---|---|---|---|
| | (v) Kwa udanganyifu kuweka karatasi tofauti na karatasi iliyoidhinishwa kisheria ndani ya sanduku la kura. | 121(1)(e) | |
| | (vi) Kutoa karatasi yoyote ya kura nje ya kituo au kukutwa na karatasi yoyote ya kura nje ya kituo cha kupigia kura. | 121(1)(f) | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | (vii) Kuharibu, kuchukua, kufungua au kuzuia sanduku lolote la kupigia kura au kifurushi cha karatasi za kura kinachotumika kwa ajili ya uchaguzi. | 121(1)(g) | |
| 3. | **Matangazo ya uongo ya kujitoa**<br><br>Kutamka, kuchapa au kutangaza kujitoa kwa mgombea yeyote kwa nia ya kumsaidia mgombea mwingine kushinda uchaguzi. | 122 | Kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miaka miwili (2). |
| 4. | **Vishawishi vya rushwa kwa ajili ya kujitoa**<br><br>Kushawishi au kusababisha mtu mwingine kujitoa kuwa | 123 | Kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja (1) na kisichozidi miaka mitano (5). |

| Na. | Kosa | Kifungu cha Sheria | Adhabu |
|---|---|---|---|
| | mgombea katika uchaguzi kwa malipo au kwa ahadi ya malipo na mtu yeyote ambaye atajitoa kutokana na vishawishi au ahadi hizo. | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | **Uongo**<br><br>Kutoa ushahidi wa uongo au maelezo ya uongo katika tamko la kupiga kura. | 124 | Faini isiyopungua Shilingi elfu hamsini (50,000) za Kitanzania na isiyozidi Shilingi laki moja au kifungo kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miezi kumi na mbili(12) au vyote kwa pamoja. |
| 6. | **Kutoa siri**<br><br>Kutoa siri yoyote inayohusu mgombea au mchakato wowote unaoendelea katika kituo cha kupigia kura. | 125 | Faini isiyopungua Shilingi laki moja (100,000) za Kitanzania na isiyozidi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja. |
| 7. | **Hongo au takrima**<br><br>Kutoa hongo, takrima au kurubuni. | 126 | Ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329. |

| Na. | Kosa | Kifungu cha Sheria | Adhabu |
|---|---|---|---|
| 8. | **Kuharibu matangazo au mabango**<br><br>Kuharibu, kukata, kuchafua au kuondoa tangazo lolote ambalo limewekwa kwa mujibu wa Sheria hii au nyaraka yoyote ambayo imewekwa kwa ajili ya uchaguzi kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii. | 136 | Faini isiyopungua Shilingi elfu thelathini (30,000) za Kitanzania na isiyozidi Shillingi laki moja(100,000) za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja (1) na kisichozidi miezi sita (6) au vyote kwa pamoja. |
| 9. | **Kufanya mikutano ya hadhara siku ya uchaguzi na kuonesha nembo ya chama katika kituo**<br><br>i. Kufanya mkutano siku ya kupiga kura au ndani ya jengo au eneo lolote ambapo upigaji kura katika uchaguzi unaendelea, au mahali popote ndani ya eneo la mita mia tatu ya eneo au jengo hilo.<br><br>ii. Kuvaa au kuonesha kadi, picha au nembo nyingine yoyote inayoonesha kuunga mkono mgombea fulani katika uchaguzi. | 134(1) na (2) | Faini isiyopungua Shilingi elfu hamsini (50,000) za Kitanzania na isiyozidi Shillingi laki moja(100,000) za Kitanzania. |

| Na. | Kosa | Kifungu cha Sheria | Adhabu |
|---|---|---|---|
| 10. | **Kuomba karatasi ya kura kwa jina au kadi ya mtu mwingine**<br><br>i. kuomba karatasi ya kura kwa jina la mtu mwingine iwe yuko hai au amefariki; na **ii.** kutoa kadi ya mpiga kura iliyotolewa kwa mtu mwingine ili kupiga kura. | 131 na 132 | Ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa, Sura ya 329. |

**Maswali ya tafakuri**

1. Taja adhabu ya kutoa tamko la uongo kuhusu kupotea au kuharibika kwa kadi ya mpiga kura.
2. Taja adhabu ya kuchochea au kufanya vurugu kwenye mkutano wa hadhara ili kuzuia usifanyike.
3. Taja adhabu ya kuondoa tangazo linalohusu uchaguzi na lililowekwa kwa mujibu wa sheria.

***KIAMBATISHO***

Idadi ya Majimbo ya Uchaguzi Mwaka 2015 - 2025

Idadi ya Majimbo ya Uchaguzi kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi Mwaka 2025 ni mia mbili na sabini na mbili (272). Ambapo Majimbo mia mbili na ishirini na mbili (222) yapo Tanzania Bara na Majimbo hamsini (50) yapo Tanzania Zanzibar. Majina ya Majimbo kwa kila Mkoa ni kama yanavyoonekana katika jedwali.

| Na. | MKOA | Na. | HALMASHAURI | Na. | JIMBO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ARUSHA | 1. | JIJI LA ARUSHA | 1. | ARUSHA MJINI |
| | | 2. | WILAYA YA ARUSHA | 2. | ARUMERU MAGHARIBI |
| | | 3. | WILAYA YA KARATU | 3. | KARATU |
| | | 4. | WILAYA YA LONGIDO | 4. | LONGIDO |
| | | 5. | WILAYA YA MERU | 5. | ARUMERU MASHARIKI |
| | | 6. | WILAYA YA MONDULI | 6. | MONDULI |
| | | 7. | WILAYA YA NGORONGORO | 7. | NGORONGORO |
| 2. | DAR ES SALAAM | 8. | JIJI LA DAR ES SALAAM | 8. | SEGEREA |
| | | | | 9. | ILALA |
| | | | | 10. | UKONGA |
| | | | | 11. | KIVULE |
| | | 9. | MANISPAA YA KINONDONI | 12. | KAWE |
| | | | | 13. | KINONDONI |
| | | 10. | MANISPAA YA UBUNGO | 14. | KIBAMBA |
| | | | | 15. | UBUNGO |
| | | 11. | MANISPAA YA KIGAMBONI | 16. | KIGAMBONI |
| | | 12. | MANISPAA YA TEMEKE | 17. | MBAGALA |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 13. | | 18. | CHAMAZI |
| | | | | 19. | TEMEKE |
| 3. | DODOMA | 14. | WILAYA YA KONDOA | 20. | KONDOA |

| **Na.** | **MKOA** | **Na.** | **HALMASHAURI** | **Na.** | **JIMBO** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 15. | JIJI LA DODOMA | 21. | DODOMA MJINI |
| | | | | 22. | MTUMBA |
| | | 16. | MJI KONDOA | 23. | KONDOA MJINI |
| | | 17. | WILAYA YA BAHI | 24. | BAHI |
| | | 18. | WILAYA YA CHAMWINO | 25. | CHAMWINO |
| | | | | 26. | MTERA |
| | | 19. | WILAYA YA CHEMBA | 27. | CHEMBA |
| | | 20. | WILAYA YA KONGWA | 28. | KONGWA |
| | | 21. | WILAYA YA MPWAPWA | 29. | KIBAKWE |
| | | | | 30. | MPWAPWA |
| 4. | GEITA | 22. | WILAYA YA GEITA | 31. | BUSANDA |
| | | | | 32. | KATORO |
| | | | | 33. | GEITA |
| | | 23. | MJI WA GEITA | 34. | GEITA MJINI |
| | | 24. | WILAYA YA NYANG'HWALE | 35. | NYANG'HWALE |
| | | 25. | WILAYA YA BUKOMBE | 36. | BUKOMBE |
| | | 26. | WILAYA YA CHATO | 37. | CHATO KASKAZINI |
| | | | | 38. | CHATO KUSINI |
| | | 27. | WILAYA YA MBOGWE | 39. | MBOGWE |
| 5. | | 28. | MANISPAA YA IRINGA | 40. | IRINGA MJINI |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | IRINGA | 29. | MJI WA MAFINGA | 41. | MAFINGA MJINI |
| | | 30. | WILAYA YA IRINGA | 42. | ISIMANI |
| | | | | 43. | KALENGA |
| | | 31. | WILAYA YA KILOLO | 44. | KILOLO |
| | | 32. | WILAYA YA MUFINDI | 45. | MUFINDI KASKAZINI |

| **Na.** | **MKOA** | **Na.** | **HALMASHAURI** | **Na.** | **JIMBO** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 46. | MUFINDI KUSINI |
| 6. | KAGERA | 33. | WILAYA YA MULEBA | 47. | MULEBA KUSINI |
| | | | | 48. | MULEBA KASKAZINI |
| | | 34. | MANISPAA YA BUKOBA | 49. | BUKOBA MJINI |
| | | 35. | WILAYA YA BIHARAMULO | 50. | BIHARAMULO MAGHARIBI |
| | | 36. | WILAYA YA BUKOBA | 51. | BUKOBA VIJIJINI |
| | | 37. | WILAYA YA KARAGWE | 52. | KARAGWE |
| | | 38. | WILAYA YA KYERWA | 53. | KYERWA |
| | | 39. | WILAYA YA MISSENYI | 54. | MISSENYI |
| | | 40. | WILAYA YA NGARA | 55. | NGARA |
| 7. | KASKAZINI PEMBA | 41. | WILAYA YA MICHEWENI | 56. | WINGWI |
| | | | | 57. | KONDE |
| | | | | 58. | MICHEWENI |
| | | | | 59. | TUMBE |
| | | 42. | WILAYA YA WETE | 60. | GANDO |
| | | | | 61. | KOJANI |
| | | | | 62. | PANDANI |
| | | | | 63. | MTAMBWE |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 64. | WETE |
| 8. | KASKAZINI UNGUJA | 43. | WILAYA YA KASKAZINI A | 65. | CHAANI |
| | | | | 66. | KIJINI |
| | | | | 67. | MKWAJUNI |
| | | | | 68. | NUNGWI |
| | | | | 69. | TUMBATU |
| | | 44. | WILAYA YA KASKAZINI B | 70. | MAHONDA |
| | | | | 71. | BUMBWINI |
| | | | | 72. | MTONI |

| **Na.** | **MKOA** | **Na.** | **HALMASHAURI** | **Na.** | **JIMBO** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 73. | DONGE |
| 9. | KATAVI | 45. | WILAYA YA MPIMBWE | 74. | KAVUU |
| | | 46. | MANISPAA YA MPANDA | 75. | MPANDA MJINI |
| | | 47. | WILAYA YA MLELE | 76. | KATAVI |
| | | 48. | WILAYA YA MPANDA | 77. | TANGANYIKA |
| | | 49. | WILAYA YA NSIMBO | 78. | NSIMBO |
| 10. | KIGOMA | 50. | WILAYA YA UVINZA | 79. | KIGOMA KUSINI |
| | | 51. | MANISPAA YA KIGOMA UJIJI | 80. | KIGOMA MJINI |
| | | 52. | MJI WA KASULU | 81. | KASULU MJINI |
| | | 53. | WILAYA YA BUHIGWE | 82. | BUHIGWE |
| | | 54. | WILAYA YA KAKONKO | 83. | KAKONKO |
| | | 55. | WILAYA YA KASULU | 84. | KASULU VIJIJINI |
| | | 56. | WILAYA YA KIBONDO | 85. | MUHAMBWE |
| | | 57. | WILAYA YA KIGOMA | 86. | KIGOMA KASKAZINI |
| 11. | KILIMANJARO | 58. | WILAYA YA SAME | 87. | SAME MASHARIKI |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 88. | SAME MAGHARIBI |
| | | 59. | MANISPAA YA MOSHI | 89. | MOSHI MJINI |
| | | 60. | WILAYA YA HAI | 90. | HAI |
| | | 61. | WILAYA YA MOSHI | 91. | MOSHI VIJIJINI |
| | | | | 92. | VUNJO |
| | | 62. | WILAYA YA MWANGA | 93. | MWANGA |
| | | 63. | WILAYA YA ROMBO | 94. | ROMBO |
| | | 64. | WILAYA YA SIHA | 95. | SIHA |
| 12. | KUSINI PEMBA | 65. | WILAYA YA CHAKE CHAKE | 96. | CHAKECHAKE |
| | | | | 97. | CHONGA |
| | | | | 98. | OLE |
| | | | | 99. | WAWI |

| Na. | MKOA | Na. | HALMASHAURI | Na. | JIMBO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 100. | ZIWANI |
| | | 66. | WILAYA YA MKOANI | 101. | CHAMBANI |
| | | | | 102. | KIWANI |
| | | | | 103. | MKOANI |
| | | | | 104. | MTAMBILE |
| 13. | KUSINI UNGUJA | 67. | WILAYA YA KATI | 105. | CHWAKA |
| | | | | 106. | TUNGUU |
| | | | | 107. | UZINI |
| | | 68. | WILAYA YA KUSINI | 108. | MAKUNDUCHI |
| | | | | 109. | PAJE |
| 14. | LINDI | 69. | MANISPAA YA LINDI | 110. | MCHINGA |
| | | | | 111. | LINDI MJINI |
| | | 70. | WILAYA YA KILWA | 112. | KILWA KASKAZINI |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 113. | KILWA KUSINI |
| | | 71. | WILAYA YA MTAMA | 114. | MTAMA |
| | | 72. | WILAYA YA LIWALE | 115. | LIWALE |
| | | 73. | WILAYA YA NACHINGWEA | 116. | NACHINGWEA |
| | | 74. | WILAYA YA RUANGWA | 117. | RUANGWA |
| 15. | MANYARA | 75. | MJI WA BABATI | 118. | BABATI MJINI |
| | | 76. | WILAYA YA HANANG | 119. | HANANG |
| | | 77. | MJI WA MBULU | 120. | MBULU MJINI |
| | | 78. | WILAYA YA BABATI | 121. | BABATI VIJIJINI |
| | | 79. | WILAYA YA KITETO | 122. | KITETO |
| | | 80. | WILAYA YA MBULU | 123. | MBULU VIJIJINI |
| | | 81. | WILAYA YA SIMANJIRO | 124. | SIMANJIRO |
| 16. | MARA | 82. | MJI WA BUNDA | 125. | BUNDA MJINI |
| | | 83. | MJI WA TARIME | 126. | TARIME MJINI |

| Na. | MKOA | Na. | HALMASHAURI | Na. | JIMBO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 84. | MANISPAA YA MUSOMA | 127. | MUSOMA MJINI |
| | | 85. | WILAYA YA BUNDA | 128. | BUNDA |
| | | | | 129. | MWIBARA |
| | | 86. | WILAYA YA BUTIAMA | 130. | BUTIAMA |
| | | 87. | WILAYA YA MUSOMA | 131. | MUSOMA VIJIJINI |
| | | 88. | WILAYA YA RORYA | 132. | RORYA |
| | | 89. | WILAYA YA SERENGETI | 133. | SERENGETI |
| | | 90. | WILAYA YA TARIME | 134. | TARIME |
| 17. | SONGWE | 91. | MJI WA TUNDUMA | 135. | TUNDUMA |
| | | 92. | WILAYA YA ILEJE | 136. | ILEJE |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 93. | WILAYA YA MBOZI | 137. | VWAWA |
| | | | | 138. | MBOZI |
| | | 94. | WILAYA YA MOMBA | 139. | MOMBA |
| | | 95. | WILAYA YA SONGWE | 140. | SONGWE |
| 18. | MBEYA | 96. | JIJI LA MBEYA | 141. | MBEYA MJINI |
| | | | | 142. | UYOLE |
| | | 97. | WILAYA YA BUSOKELO | 143. | BUSOKELO |
| | | 98. | WILAYA YA CHUNYA | 144. | LUPA |
| | | 99. | WILAYA YA KYELA | 145. | KYELA |
| | | 100. | WILAYA YA MBARALI | 146. | MBARALI |
| | | 101. | WILAYA YA MBEYA | 147. | MBEYA VIJIJINI |
| | | 102. | WILAYA YA RUNGWE | 148. | RUNGWE |
| 19. | MJINI MAGHARIBI | 103. | WILAYA YA MAGHARIBI A | 149. | BUBUBU |
| | | | | 150. | WELEZO |
| | | | | 151. | MFENESINI |
| | | | | 152. | MWERA |
| | | 104. | WILAYA YA MAGHARIBI B | 153. | DIMANI |
| | | | | 154. | FUONI |

| **Na.** | **MKOA** | **Na.** | **HALMASHAURI** | **Na.** | **JIMBO** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 155. | KIEMBE SAMAKI |
| | | | | 156. | MWANAKWEREKWE |
| | | | | 157. | PANGAWE |
| | | 105. | WILAYA YA MJINI | 158. | AMANI |
| | | | | 159. | CHUMBUNI |
| | | | | 160. | JANG'OMBE |
| | | | | 161. | KIKWAJUNI |

| Na. | MKOA | Na. | HALMASHAURI | Na. | JIMBO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 162. | KWAHANI |
| | | | | 163. | MAGOMENI |
| | | | | 164. | MALINDI |
| | | | | 165. | MPENDAE |
| | | | | 166. | SHAURIMOYO |
| 20. | MOROGORO | 106. | MJI IFAKARA | 167. | KILOMBERO |
| | | 107. | MANISPAA YA MOROGORO | 168. | MOROGORO MJINI |
| | | 108. | WILAYA YA GAIRO | 169. | GAIRO |
| | | 109. | WILAYA YA MLIMBA | 170. | MLIMBA |
| | | 110. | WILAYA YA KILOSA | 171. | KILOSA |
| | | | | 172. | MIKUMI |
| | | 111. | WILAYA YA MOROGORO | 173. | MOROGORO KUSINI |
| | | | | 174. | MOROGORO KUSINI MASHARIKI |
| | | 112. | WILAYA YA MVOMERO | 175. | MVOMERO |
| | | 113. | WILAYA YA ULANGA | 176. | ULANGA |
| | | 114. | WILAYA YA MALINYI | 177. | MALINYI |
| 21. | MTWARA | 115. | WILAYA YA MTWARA | 178. | MTWARA VIJIJINI |
| | | 116. | MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI | 179. | MTWARA MJINI |
| | | 117. | MJI WA MASASI | 180. | MASASI MJINI |
| | | 118. | MJI WA NANYAMBA | 181. | NANYAMBA |
| | | 119. | MJI WA NEWALA | 182. | NEWALA MJINI |
| | | 120. | WILAYA YA MASASI | 183. | LULINDI |
| | | | | 184. | NDANDA |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 121. | WILAYA YA NANYUMBU | 185. | NANYUMBU |
| | | 122. | WILAYA YA NEWALA | 186. | NEWALA VIJIJINI |
| | | 123. | WILAYA YA TANDAHIMBA | 187. | TANDAHIMBA |
| 22. | MWANZA | 124. | MANISPAA YA ILEMELA | 188. | ILEMELA |
| | | 125. | JIJI LA MWANZA | 189. | NYAMAGANA |
| | | 126. | WILAYA YA BUCHOSA | 190. | BUCHOSA |
| | | 127. | WILAYA YA KWIMBA | 191. | KWIMBA |
| | | | | 192. | SUMVE |
| | | 128. | WILAYA YA MAGU | 193. | MAGU |
| | | 129. | WILAYA YA MISUNGWI | 194. | MISUNGWI |
| | | 130. | WILAYA YA SENGEREMA | 195. | SENGEREMA |
| | | 131. | WILAYA YA UKEREWE | 196. | UKEREWE |
| 23. | NJOMBE | 132. | MJI WA MAKAMBAKO | 197. | MAKAMBAKO |
| | | 133. | MJI WA NJOMBE | 198. | NJOMBE MJINI |
| | | 134. | WILAYA YA LUDEWA | 199. | LUDEWA |
| | | 135. | WILAYA YA MAKETE | 200. | MAKETE |
| | | 136. | WILAYA YA NJOMBE | 201. | LUPEMBE |
| | | 137. | WILAYA YA WANGING'OMBE | 202. | WANGING'OMBE |
| 24. | PWANI | 138. | MJI WA KIBAHA | 203. | KIBAHA MJINI |
| | | 139. | WILAYA YA BAGAMOYO | 204. | BAGAMOYO |

| **Na.** | **MKOA** | **Na.** | **HALMASHAURI** | **Na.** | **JIMBO** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 140. | WILAYA YA CHALINZE | 205. | CHALINZE |
| | | 141. | WILAYA YA KIBAHA | 206. | KIBAHA VIJIJINI |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 142. | WILAYA YA KISARAWE | 207. | KISARAWE |
| | | 143. | WILAYA YA MAFIA | 208. | MAFIA |
| | | 144. | WILAYA YA MKURANGA | 209. | MKURANGA |
| | | 145. | WILAYA YA KIBITI | 210. | KIBITI |
| | | 146. | WILAYA YA RUFIJI | 211. | RUFIJI |
| 25. | RUKWA | 147. | MANISPAA YA SUMBAWANGA | 212. | SUMBAWANGA MJINI |
| | | 148. | WILAYA YA KALAMBO | 213. | KALAMBO |
| | | 149. | WILAYA YA NKASI | 214. | NKASI KASKAZINI |
| | | | | 215. | NKASI KUSINI |
| | | 150. | WILAYA YA SUMBAWANGA | 216. | KWELA |
| 26. | RUVUMA | 151. | WILAYA YA NYASA | 217. | NYASA |
| | | 152. | WILAYA YA SONGEA | 218. | PERAMIHO |
| | | 153. | MANISPAA YA SONGEA | 219. | SONGEA MJINI |
| | | 154. | MJI WA MBINGA | 220. | MBINGA MJINI |
| | | 155. | WILAYA YA MADABA | 221. | MADABA |
| | | 156. | WILAYA YA MBINGA | 222. | MBINGA VIJIJINI |
| | | 157. | WILAYA YA NAMTUMBO | 223. | NAMTUMBO |
| | | 158. | WILAYA YA TUNDURU | 224. | TUNDURU KASKAZINI |
| | | | | 225. | TUNDURU KUSINI |
| 27. | SHINYANGA | 159. | MANISPAA YA SHINYANGA | 226. | SHINYANGA MJINI |
| | | 160. | MANISPAA YA KAHAMA | 227. | KAHAMA MJINI |

| Na. | MKOA | Na. | HALMASHAURI | Na. | JIMBO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 161. | WILAYA YA KISHAPU | 228. | KISHAPU |
| | | 162. | WILAYA YA MSALALA | 229. | MSALALA |
| | | 163. | WILAYA YA SHINYANGA | 230. | SOLWA |
| | | | | 231. | ITWANGI |
| | | 164. | WILAYA YA USHETU | 232. | USHETU |
| 28. | SIMIYU | 165. | WILAYA YA BARIADI | 233. | BARIADI VIJIJINI |
| | | 166. | MJI WA BARIADI | 234. | BARIADI MJINI |
| | | 167. | WILAYA YA BUSEGA | 235. | BUSEGA |
| | | 168. | WILAYA YA ITILIMA | 236. | ITILIMA |
| | | 169. | WILAYA YA MASWA | 237. | MASWA MAGHARIBI |
| | | | | 238. | MASWA MASHARIKI |
| | | 170. | WILAYA YA MEATU | 239. | KISESA |
| | | | | 240. | MEATU |
| 29. | SINGIDA | 171. | MANISPAA YA SINGIDA | 241. | SINGIDA MJINI |
| | | 172. | WILAYA YA IKUNGI | 242. | IKUNGI MAGHARIBI |
| | | | | 243. | IKUNGI MASHARIKI |
| | | 173. | WILAYA YA IRAMBA | 244. | IRAMBA MAGHARIBI |
| | | 174. | WILAYA YA ITIGI | 245. | ITIGI |
| | | 175. | WILAYA YA MANYONI | 246. | MANYONI |
| | | 176. | WILAYA YA MKALAMA | 247. | IRAMBA MASHARIKI |
| | | 177. | WILAYA YA SINGIDA | 248. | ILONGERO |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 30. | TABORA | 178. | WILAYA YA KALIUA | 249. | KALIUA |
| | | | | 250. | ULYANKULU |
| | | 179. | WILAYA YA URAMBO | 251. | URAMBO |
| **Na.** | **MKOA** | **Na.** | **HALMASHAURI** | **Na.** | **JIMBO** |
| | | 180. | MANISPAA YA TABORA | 252. | TABORA MJINI |
| | | 181. | MJI WA NZEGA | 253. | NZEGA MJINI |
| | | 182. | WILAYA YA IGUNGA | 254. | IGUNGA |
| | | | | 255. | MANONGA |
| | | 183. | WILAYA YA NZEGA | 256. | BUKENE |
| | | | | 257. | NZEGA VIJIJINI |
| | | 184. | WILAYA YA SIKONGE | 258. | SIKONGE |
| | | 185. | WILAYA YA UYUI | 259. | IGALULA |
| | | | | 260. | UYUI |
| 31. | TANGA | 186. | MJI WA KOROGWE | 261. | KOROGWE MJINI |
| | | 187. | WILAYA YA HANDENI | 262. | HANDENI |
| | | 188. | JIJI LA TANGA | 263. | TANGA MJINI |
| | | 189. | MJI WA HANDENI | 264. | HANDENI MJINI |
| | | 190. | WILAYA YA BUMBULI | 265. | BUMBULI |
| | | 191. | WILAYA YA KILINDI | 266. | KILINDI |
| | | 192. | WILAYA YA KOROGWE | 267. | KOROGWE VIJIJINI |
| | | 193. | WILAYA YA LUSHOTO | 268. | LUSHOTO |
| | | | | 269. | MLALO |
| | | 194. | WILAYA YA MKINGA | 270. | MKINGA |
| | | 195. | WILAYA YA MUHEZA | 271. | MUHEZA |
| | | 196. | WILAYA YA PANGANI | 272. | PANGANI |